# *ILE ISHARA*

Mwaweza kuketi. Habari za asubuhi, kila mmoja wenu! Ninafurahia kuwa katika utumishi wa Bwana asubuhi ya leo, kurudi tena. . . Sikujua kama tungerudi ama la, bali Bwana alifungua njia, nasi tukarudi kwa ajili ya ibada leo. Sasa tunatarajia nyakati kuu leo, asubuhi hii, katika somo hili la Jumapili, katika Neno. Na usiku wa leo itakuwa ibada ya uponyaji tena, ikifuatiwa na ibada ya ushirika.

2 Na sasa tuna—mtoto wa kuwekwa wakfu, naamini . . . Ndugu Neville alikuwa akiniambia ya kwamba mtu fulani alikuwa na mtoto wao wa kuwekwa wakfu. Na kama watamleta mtoto huyo wakati huu, basi. Naye ndugu yetu atabaki, ama baadhi yao, kwenye kinanda ama piano, mojawapo. Kisha watamleta huyo mtoto humu. Tutafanya ibada ya kuwekwa wakfu; ili tuingie, upesi tuwezavyo, katika Neno.

3 Kwa maana, sisi hupenda ku—kudumu katika Neno. Hilo, hilo ndilo jambo muhimu, kutoa wakati wetu kabisa kwa Neno la Bwana. Kwa hivyo tunashukuru kwa nafasi hii ya kukutana nanyi nyote hapa leo, na ku . . . na hii—ibada hii.

4 Hapana budi nilikosea. Hiyo ni sawa, dada. Ni—ni—nilifikiri kulikuweko. Huenda ikawa kosa tu. Haidhuru. Basi, nakushukuru, sana, hata hivyo. Labda hii, nafikiri ilisemwa na mtu mwingine, kupitia kwa mtu mwingine, naye akalifanya kuwa ngumu.

5 Sasa kila mtu anajisikia vizuri? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] . . .?. . . Mungu asifiwe!

6 [Ndugu Neville anasema, "Ndio hawa wanakuja."—Mh.] Naam, ndio, hawa hapa hao watoto. Nasikitika. Nasikitika. Vema, njoo, mzee. ["Naam, bwana."]

7 Vema, vipi wawili, wasichana wadogo wawili na wazuri wenye macho ya kahawia! Aha? Huo ni uzuri. Jina lake ni nani? Hebu angalia! [Mamaye anasema, "Jennifer Lee."—Mh.] Jenny? ["Jennifer Le."] Jennifer Lee. Jina lake la mwisho ni nani? ["Serept."] Serept. Umetoka wapi, Dada Lee? ["Versailles, Illinois."] Versailles, Illinois. Ni vizuri namna gani!

8 Sasa, katika Biblia. Sasa, kwa kawaida, wao—wao huwabatiza watoto; hatuamini katika kuwabatiza watoto, kwa sababu hawajatenda dhambi bado, maana wao wangali wachanga mno. Bali tunaamini katika kuwaweka watoto wakfu kwa Bwana. Sasa mimi pamoja na mzee tutamwekea mikono huyu mtoto mchanga. Jenny, unasemaje? [Ndugu Neville anasema, "Jennifer."—Mh.] Jennifer. Sawa.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

9 Baba wa Mbinguni, asubuhi ya leo tunapomleta huyu msichana mchanga anayeitwa Jennifer, Kwako, mamaye na marafiki zake wamemleta kutoka mbali sana, kuwekwa wakfu kwa Bwana. Tunajua ya kwamba Wewe uliweka mikono Yako juu ya watoto kama hawa, katika siku Zako, kisha—kisha ukasema, "Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, Ufalme wa Mbinguni ni wao." Sasa tunamtoa Kwako, akakutumikie maishani mwake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

10 Jina la huyo msichana mwingine mdogo ni nani? [Mamaye anasema, "Connie Lynn."—Mh.] Connie Lynn. Sawa, Connie mdogo, unanifanya, unanifanya nijisikie mdogo. Unaogopa nini? Lo, nasikitika hilo halifai kitu, mama. Vema.

Hebu na tuviinamishe vichwa vyetu.

11 Bwana Yesu, huyu mama anamleta mtoto Connie kwetu asubuhi ya leo, katika ibada ya kumweka wakfu kwa Mwenyezi. Ulimpa mtoto huyu, kumlea, naye anamleta Kwako, pamoja na dada yake mdogo. Naomba, Baba uliye Mbinguni, ya kwamba utamrehemu. Ibariki jamaa hii. Bariki huyu msichana mdogo. Tunapomwekelea mikono, katika Jina la Yesu Kristo, tunamtoa Kwako kwa maisha ya utumishi. Amina.

Mungu akubariki, pamoja na watoto wako hapo.

Jamani, tuna watoto wengi wachanga sasa!

12 Jina la huyu mvulana mdogo ni nani? [Mamaye anasema, "Joel Lee Watson."—Mh.] Joel Watson. ["Joel Lee."] Joel Lee Watson. Ni kijana mwanamume mzuri jinsi gani, mwenye macho makubwa ya samawati! Jamani! Nyote mwatoka wapi? ["Eastman, Georgia."] Kutoka Georgia. ["Naam."] Nilifikiri ulitoka Kusini. Sikujua. ["Vema, mama yangu anakaa karibu na Tifton. Ni huko chini."] Loo, naam. Loo, habari zako! Huyu ni kijana mzuri, mtoto wa kiume wa Georgia, basi, aha? Vema, bwana. Naam, bwana, hiyo ni nzuri sana. Anaweza kunena, pia. Wewe je?

Hebu na tuviinamishe vichwa vyetu.

13 Baba wa Mbinguni, tunamleta huyu mvulana mdogo mpenzi, mamaye na babaye wanaposimama hapa ka—katika umoja wao. Umewapa hao huyu mtoto mdogo kumlea, nao wanamrudisha Kwako. Haya yangekuwa mandhari ma—mazuri vipi, kama Hana, wa kale, aliyeomba dua kwa ajili ya mtoto; na—na Mungu akampa huyo mtoto, naye kamrudisha katika hekalu la Mungu, katika kumweka wakfu. Tujalie, Bwana, ya kwamba huyu mvulana mdogo atakuwa mtumishi Wako, ya kwamba babaye na mamaye watabarikiwa, na wapate afya na nguvu kumlea. Naye na aishi maisha marefu, yenye furaha, na awe mtumishi Wako, tunapomkabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. (Akubariki!) Na umfanye mtu mzuri, yamkini nabii mwingine mdogo kama Samweli.

14 Sasa hapa kuna wavulana wawili wadogo, walio wazuri. Jamani! Watatu wao pale? Vema, hiyo ni jamaa nzima. Jina lako ni nani? [Mvulana huyo anasema, “Michael.”] Michael. Na lako? [Huyo mvulana mwingine anasema, “Paul.”] Paul. Ni majina mazuri namna gani! Na lako? [Mshichana anasema, “Debbie.”] Debra. Hilo ni nzuri kabisa. Michael, na Paul, na Debra. Na jina lako la mwisho ni nani? [Baba anasema, “Ellis.”] Ellis? [“Naam.”] Vema, hiyo ni jamaa nzuri sana, nawaambieni.

15 Mwajua, ninapowaona vijana wadogo kama hao, kila mara inanirudisha nilipokuwa mvulana mdogo. Na sasa ule msemo wa kale ni, mwajua, “Wataikanyaga miguu yako sasa, na moyo wako baadaye,” bali siamini itakuwa hivyo tu tunapowaweka wakfu kwa Bwana. Tunalo jukumu hapa, na Mungu aliliweka hili mkononi mwako. Alikufanya mhubiri. Kila mara nilinena kuhusu wahubiri wanawake, mwajua, bali kila mama ni mhubiri; ndilo hili hapa kusanyiko lake, mnaona, kuwalea hawa watoto wachanga ipasavyo, huku baba anafanya kazi. Nawe unalo jukumu. Mungu awabariki nyote wawili, mna jamaa ndogo na nzuri.

16 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja pamoja na Michael mdogo, inaonekana kana kwamba ndiye mtoto wa kwanza. Nasi tunaiweka mikono yetu juu yake, katika kumweka wakfu, kwa Yesu Kristo. Jamaa yake inawaleta watoto wao kwa maana ulimweka huyu wapate—wapate kumlea, nao wanajua ya kwamba wao hawatoshi, bila msaada Wako, kwa hivyo wanaileta jamaa yao ndogo, kuwaweka wakfu.

17 Sasa nakupa Wewe huyu mtoto Michael, akakutumikie maishani mwake, katika Jina la Yesu Kristo. Vivyo hivyo, tunaiweka mikono yetu juu ya Paul mdogo, nasi tunayaweka maisha yake wakfu kwa Yesu Kristo, apate kumtumikia maishani mwake kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Na juu ya Debra mdogo, tunaiweka mikono yetu juu yake, Baba, katika kumweka wakfu, kwa kumbukumbu la Yesu Kristo. Ambaye aliweka mikono Yake juu ya watoto wadogo, kasema, “Waacheni waje kwangu; wala msiwazuie.” Na maisha ya msichana huyu mdogo yabarikiwe katika Ufalme wa Mungu.

18 Bariki baba na mama, nao na waishi maisha marefu yenye furaha, kuwaona watoto wao katika utumishi wa Mungu. Tunaomba baraka hii kwa utukufu wa Mungu, tunapowaweka wakfu katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Akubariki! Akubariki! Ninyi ni jamaa ndogo na nzuri. Naam.

19 Nini. . .Mwajua ninayowazia? Wasichana wadogo huwa, wanapendeza sana sasa kuliko walivyokuwa nilipokuwa mvulana mdogo. Naam, bwana. Ni macho mazuri na makubwa namna gani! Jina lake ni nani? [Mamaye anasema, “Joanna.”—Mh.] Joanna. Na jina lako la mwisho ni. . .[Babaye anasema,

"Blair."] Blair, Joanna Blair. Ninyi ambao mnatazama kule nyuma, si yeye ni mrembo? Naam, bwana. Nawe habari zako, Joanna, aha? Ana haya kidogo, Joanna, ana haya kidogo. Mtoto mchanga mzuri.

Hebuni tuviinamishe vichwa vyetu.

20 Baba wa Mbinguni, jamaa hii ya Blairs ilipewa hawa kwa ndoa yao, huyu Joanna mdogo. Nasi tunajua ya kwamba siku hizi ni bovu, wakati Shetani yuko kila mahali, kuvizia, hasa sana hawa wasichana wadogo. Nao wanajua ya kwamba hawatoshi ku—kumlea ipasavyo. Nao wanamtaka alewe impasavyo, na awe mtumishi Wako. Nao wanamlea huyu msichana mdogo apate kukuheshimu Wewe. Na sasa wanamleta, katika kuwekwa kwake wakfu, Kwako. Tunaiweka mikono yetu juu yake, katika Jina la Yesu Kristo, tunapomweka wakfu mtoto Joanna Blair kwa Ufalme wa Mungu, kwa utukufu wa Mungu. Amina.

Ubarikiwe, Ndugu Blair. Bwana awe pamoja nawe.

21 Habari za asubuhi, bwana! [Baba anasema, "Nzuri!"—Mh.] Huyu ni mvulana mzuri jinsi gani! Ewe, u hali gani? Vema, jamani, unaonekana mzuri zaidi kama ukigeuka upande *huu*. Naam, bwana. Una kichwa kidogo, kizuri, cha kupendeza sana, na uso unaoambatana nacho. Aha? Jina lako ni nani? ["Daniel Mark."] Daniel Mark. Na la mwisho? ["Mark Harden,"] Harden. ["Harden."] Harden, Daniel Mark Harden.

22 Umetoka eneo hili, Ndugu Harden? [Ndugu Harden anasema, "Sasa, jiji la Melkerk."—Mh.] Naam, bwana. Unatoka wapi? ["Mimi ni mwenyeji wa Jimbo la New York"] Kutoka Jimbo la New York. Yankee hasa. ["Ndivyo."] Vema, ni jimbo kuu. Nina watu wanaoishi kule. Mjomba wangu huishi Plattsburgh. Lo, nimefurahiwa sana kule New York. Nitaenda huko kwa mkutano wangu ujao, Jiji la New York, katika lile kanisa la mawe. Vema.

23 Sasa, jina lake ni Mark, unasema? [Babaye asema, "Daniel Mark."—Mh.] Daniel Mark, mvulana mdogo mzuri namna gani!

Na tuviinamishe vichwa vyetu.

24 Bwana Yesu, tunakuletea mtoto Daniel Mark, katika kuyaweka maisha yake wakfu. Ametolewa mikononi mwa baba na mama, kumlea mtoto huyu mdogo katika maonyo ya Mungu. Nao wanajua ya kwamba hawatoshi, kwa hivyo wanamleta Kwako, Bwana, upate kuyabariki maisha yake. Na, sasa, nasi tunajua ya kwamba siku hizi tumamoishi ni baya. Tunawaona watoto wadogo, hatujui kesho inayo nini, lakini, hata iwe nini, tunayaaminisha mkononi Mwako. Tunamwekea mikono huyu mvulana mdogo, na kuyaweka maisha yake wakfu Kwako, apate kukutumikia maishani katika Ufalme wa Mungu, katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

25 Mungu akubariki, ndugu. Yeye ni mvulana mzuri. Na ubarikiwe, Mark mdogo.

> Lo . . . walete, walete,
> Kutoka dhambini walete;
> Lo, walete, walete;
> Na walete kwake Yesu.

Hiyo ni ajabu! Asante, dada.

26 Wangapi walikuwa hapa Jumapili, mlioombewa Jumapili iliyopita, wanaona matokeo yake na mnajua mmeponywa? Inueni mikono yenu, walioombewa. Lo, jamani, angalieni hapa, karibu kila mmoja wao.

27 [Ndugu Neville anasema, "Haleluya! Si ajabu hiyo! Mungu asifiwe! Nimekuwa nikisikia habari zake, juma nzima."—Mh.] Naam, bwana. Mimi pia. Nataka tu niketi, nikisikiza, mnaona.

28 Mnaona, jambo fulani linatendeka, ambalo nitawaambieni baadaye. Kwa hivyo, sasa, mnaona, ni—ni lenye utukufu na la ajabu. Na kama sisi . . . Tutanena hayo, katika mkutano mwingine, mnajua, wakati fulani. Linaanza sasa kutendeka, nasi tunashukuru kwa hilo.

29 Nimekuwa kule Kentucky, kama nifanyavyo kila mwaka, kwenda huko. Nilikuwa na baadhi ya marafiki zangu kule. Na si kuwinda kindi pekee, nanyi mwajua hayo, mnaona.

30 Kwa hivyo tuna wakati mtukufu sana, nasi tunamshukuru Bwana.

31 Sina budi kwenda sasa, kwenda nyumbani baada ya mkutano huu. Ndiposa nasi tuta . . . Kisha nitarudi huku tena baada ya kitambo kidogo, nikienda New York kwa ajili ya mkutano. Nasi tukipata nafasi ya kukaa kwa kitambo kidogo, kwani, tu—tutafurahia kuwa na mkutano mwingine hapa, Maskanini.

32 Kisha sina budi kurudi, kwenda Shreveport. Ndipo tutakaporudi nyumbani, na kutumainia kuwa hapa likizoni, Bwana akipenda, kuwarudisha jamaa yangu. Kisha—kisha nataka ku . . .

33 Halafu mkutano wangu utakuwa kule Phoenix, Januari. Ni mkutano wa mwaka wa Wafanyi Biashara Wakristo. Na yapata juma moja ama siku kumi kabla ya hapo, nitajaribu ku—kuazima lile kubwa . . . Watu wa Jina la Yesu; ilikuwa Ndugu Garcia, na yu—yule Ndugu Mhispaniola pale walikuwa na mahali pakubwa ajabu. Walipajenga hivi majuzi. Patakaa watu elfu kadha, papya kabisa, na kusanyiko lao ni ndogo sana. Waliniambia naweza kupakodisha wakati wo wote nitakao. Badala ya kwenda kila ma—mahali, kuzunguka hilo bonde, kanisa baadaye kanisa, nafikiri nitayaunganisha yote katika mkutano mmoja mkuu wa muungano, mwaona, kisha niufanye pale.

34 Ndiposa tunaweza kukodisha hilo hekalu. Tunaenda kuangalia hivi sasa kama tunaweza, ndiposa tuwe na Mkutano wa Wafanyi Biashara Wakristo. Halafu, mpaka ya nchi za ng'ambo yatakaponyoshwa, tutajaribu kutayarisha mikutano sehemu za Kusini, mnamo Januari, Februari na Marchi, huko nyanda za Kusini. Kisha—kisha niende. . .maana, tukianza sasa na kuenda Afrika. . .Mnaona, wakati huu wa Krisimasi, kwao, ni Julai nne. Angalia, ku—kuna mvua nyingi na ni kubaya, na hauwezi kuingia kule, wakati huo, kwa hivyo wakati mzuri sana wa kwenda kule ni baadaye. Ndiposa tunataka kuanzia, tukiweza, huko Norway, na kushuka tukizunguka kote ulimwenguni, kisha tuingie Afrika, tumalizie huko, Bwana akipenda.

35 Lakini na tuombeeni sasa. Nasi tunawapenda, nanyi mwajua hivyo. Kwa hiyo tunatarajia mambo ya ajabu mno, kuliko yote tungeliweza kufanya, ama hata kuwazia Bwana angetenda.

36 Nasi tunaamini, usiku wa leo, kutakuweko na ibada kuu ya uponyaji; ninaamini kutakuweko na. . .sitasema ila kidogo tu, kwani tuna ushirika usiku wa leo. Na kwa hivyo kama dakika ishirini ama thelathini hivi, ndiposa tutafanya mstari wa maombi, na—na kisha mara baada ya hayo, tutakuwa—tutakuwa na ushirika. Nanyi mmekaribishwa kukaa pamoja nasi; tutafurahia. Hatuna ushirika wa ya—faragha. Ni kwa kila mwamini, kila mwamini.

37 Na kabla sijasoma Maandiko, nashangaa kama tungeliinamisha vichwa vyetu kwa muda mfupi. Nitamuuliza rafiki yangu mpenzi, Ndugu Lee Vayle, kama atatuongoza kwa maombi, ili Bwana alibariki Neno Lake. Ndugu Vayle, utatufanyia hivyo? [Ndugu Vayle sasa anaomba—Mh.] Amina. Tujalie, Bwana. Tujalie, Bwana. Tujalie, Bwana. Naam, Bwana. Amina.

38 Sasa kwa heshima, na kicho, tunalikaribia Neno. Sasa ningependa kusoma, asubuhi hii, kutoka Kutoka sura ya 12, na kuanzia kifungu cha 12, kifungu cha 12 na 13, vyote pamoja. Nanyi sikizeni kwa makini sana sasa. Kisha kabla ya ushirika usiku wa leo, someni sura ya 12 ya—ya Kutoka, sura nzima; kwa kuwa kifungu cha 11 hapa ni kujitayarisha kwa ajili ya safari, na ushirika kabla ya ile safari. Nasi tunataka kuyaendea haya kwa unyenyekevu sana sasa. Basi aya ya 12 ya sura ya 12:

> *Maana nitapita kati ya nchi ya Misri usiku huu, nami*
>
> *nitawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, wa wanadamu na wa wanyama; nami nitafanya hukumu juu ya miungu yote ya Misri; Mimi ndimi BWANA.*
>
> *Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile nyumba mtakazokuwamo; nami nitakapoiona ile damu,*

*nitapita juu yenu. Lisiwapige pigo to lote likawaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri.*

39 Bwana na abariki Neno Lake Takatifu!

40 Sasa, nataka kuchukua somo kutoka hapo, neno moja tu lenye herufi tano: *(Token) Ishara*. Ishara! Nataka kunena juu ya neno, ama kufundisha somo hili la shule ya Jumapili, juu ya neno "ishara." Biblia ilisema hapa, "Na ile damu itakuwa ishara kwenu." Nasi tunataka kutumia hilo neno, "ishara."

41 Sasa hatujui; ninapoangalia saa, na wakati unapofika, vema, haya ni . . . Nina Maandiko mengi, mengi sana yaliyoandikwa hapa. Kwa hivyo sio . . . Na nikijua ya kwamba sitakuwa pamoja nanyi kwa muda. Na tunajuaje ya kwamba huu hautakuwa wakati wa mwisho kwa wengine wetu kukutana pamoja, kwa hivyo, hebuni tujaribu kuliendea kwa unyenyekevu sana. Najua hilo ni gumu. Bwana ametupa asubuhi njema, pia—pia, kwa ibada, njema tu. Basi hebuni tujaribu kutilia maanani sana kila kitu ambacho—ambacho tutazungumzia, kusudi . . . iwapo mna cho chote mle ambacho Bwana angetaka mjue, ili muweze kupewa.

42 Na hatusimami hapa kuonekana tu. Hatuji hapa kusudi watu wengine waone nguo tulizovaa. Ama . . . Sisi, tunakuja hapa, kwa kusudi moja, kama Ndugu yetu alivyoomba lile ombi, "Tuko hapa, kulisikia Neno, Neno likitujia sisi." Tunataka Hilo, kwa sababu hilo ndilo kitu pekee kitakachomaanisha cho chote kwetu, cho chote kitakachokuwa cha maana, cho chote ambacho—ambacho kitatusaidia.

43 Nasi ni watu wenye kufa. Binadamu wote wanaelekea Umilele. Ndiposa huu ndio wakati tulio nao wa kujiamulia tutaelekea njia ipi. Barabara iko mbele yetu; tunaweza kuchukua upande wo wote tunaotaka kuchagua. Hivyo ndivyo alivyowaweka Adamu na Hawa, na hivyo ndivyo anavyotuweka sisi.

44 Yatupasa kukumbuka, ya kwamba hata tufanyeje ama tumefanikiwa vipi, maishani, bila Kristo tumepoteza kila kitu kabisa. Basi kama Yeye, baada . . . Iwapo Yeye ndiye yote yaliyopo ya kutazamia, basi sisi tungekuwa ndio watu walio wapumbavu sana kutokulikubali, kuwa, na—na kulipenda. Si kulikubali tu, bali unafikia jambo kuu kuliko hilo. Baada ya kulipata, usilichukue na kuliweka kabatini—huna budi kulitumia.

45 Ni kama kwenda kwa daktari kupata dawa, kisha ukaziweka kabatini. Ukienda kuchukua dawa, zinywe. Iwapo kuna ugonjwa unaokusumbua, na dawa hii inakusudiwa kukusaidia, basi kunywa akupacho; na jinsi asemavyo itumiwe, kwa maana wakati mwingine dakika chache tu huleta tofauti sana jinsi unavyoitumia. Na jinsi tujuavyo . . .

46 Basi kwa hali hii, leo uamuzi wako wa muda kidogo tu huenda ukaamua kikomo chako cha Milele. Lichukue tu jinsi anavyokupa.

Ishara, "Ile damu itakuwa ishara kwenu."

47 Sasa, kwanza, ishara ni nini? Ni neno linalotumika kwa kawaida kati yetu sisi watu tunaozungumza Kiingereza, zaidi sana hapa Amerika. Ishara ni . . . Kwa kweli, kamusi inasema ishara ni dalili, ni dalili ya nauli, gharama iliyolipwa, mwaona, ya kwamba na—nauli, ama gharama, gharama inayohitajika ambayo imekwisha lipwa.

48 Kama nauli ya gari la moshi ama ya gari la abiria. Unaondoka unaenda unalipa nauli ya—yako, kisha wanakupa tikiti, na hiyo tikiti haiwezi kutumika kwa cho chote kingine, ila gari la moshi. Na ni ishara, kwa kampuni ya reli, ya kwamba tayari umelipa nauli yako. Ni ishara, na hauwezi kuitumia kwa njia nyingine yo yote. Haitumiki kwa shirika lingine lo lote. Inatumika kwa shirika hilo tu. Nayo ni—ni ishara.

49 Basi humu ndani, tunayoyasema, tunapoanzia, ni Mungu akiwaambia Israeli, "Damu ya mwana-kondo ndiyo ishara kwenu." Mwana-kondoo wa Israeli, aliyechinjwa, ndiyo ishara aliyohitaji Yehova. Haina budi kuwa damu. Mungu alifanya ishara na kuwapa Israeli. na hamna ishara nyingine itakayokubalika, waona, haiwezi kutambuliwa.

50 Kwa ulimwengu, Hiyo ni upuzi mtupu. Bali, kwa Mungu, ndiyo njia pekee. Kitu pekee Yeye anachohitaji tu ni ile Ishara. Haina budi kuweko. Nawe hauwezi kuwa na ile Ishara hata nauli iwe imelipwa, ndipo u mwenyeji wa Ishara ambayo inakupa he—heshima ya Pasi ya bure. "Nitakapoiona ile Damu, nitapita juu yenu." Ni wakati jinsi gani, huo, ni heshima jinsi gani, kujua ya kwamba unabeba, ndani mwako, Pasi. "Nitakapoiona ile Damu, nitapita juu yenu." Ndicho kitu pekee ambacho Yeye atatambua. Hamna kingine kinachoweza kuchukua mahali pake; hamna cha kubadilisha, hamna dhehebu, hamna cho chote kingine. Hiyo ndiyo inayohitajika. Mungu alisema, "Hiyo peke yake ndiyo nitakayoangalia peke yake."

51 Haidhuru walikuwa wenye haki vipi, jinsi gani walivyokuwa wema, jinsi walivyokuwa na elimu nyingi, jinsi walivyovaa, Ishara ilikuwa ndiyo kitu pekee. "Nitakapoiona ile ishara, nitapita juu yenu." Ile damu ilikuwa Ishara ya kwamba ma—masharti ya Yehova yalikuwa yametimizwa, ya kwamba yamekwisha tekelezwa. Ile damu iliwakilisha ishara. Ile damu ilikuwa ndiyo ishara. Mnaona? Ule uhai ambao . . .

52 Mungu alikuwa tayari amesema, "Siku utakayokula matunda ya mti huo, utakufa siku hiyo." Na kulikuwa na uhai ulioondolewa badala ya uhai wa mwamini. Mungu, katika rehema, alikubali kitu kingine badala ya uhai wa mtu aliyetiwa unajisi. Wakati mwanawe alipojitia unajisi kwa dhambi, ya

kutokuamini Neno, ndipo Mungu, aliye mwingi wa rehema, akampa kitu kingine; na, hicho kilikuwa, kitu fulani kilipaswa kufa badala yake. Hamna kingine kingelifaa.

53 Hiyo ndiyo sababu yale matofaa na matunda kama maembe ya Kaini, na kadhalika, hayakufaa kitu. Ilipaswa kuwa uhai uliokuwa na damu, nao huo uhai ulikuwa umetoka kwenye hiyo sadaka, sasa damu ilikuwa ishara ya kwamba agizo la Mungu limetimizwa. Basi, Mungu alihitaji nini? Uhai; nayo ile damu ilionyesha ya kwamba hapana budi uhai fulani ulikuwa tayari umetoka. Kwa hivyo ile damu ilikuwa ishara ya kwamba uhai ulikwisha tolewa, ya kwamba kitu fulani kimekufa, masharti ya Mungu; ya kwamba uhai tayari umetolewa, na damu imemwagika. Nayo ile damu iliwakilisha ishara, ya kwamba ule uhai ulikuwa umetoka. Uhai wa mnyama ambao Mungu alikuwa ameagiza utolewe, ilikuwa ile damu iliyowakilisha ile ishara. Mnaona?

54 Mwa—mwa—mwabudu aliyeamini alitambulishwa pamoja na sadaka yake, kwa ile ishara. Sitaki kuchukua muda mrefu sana katika matamshi haya madogo; bali, ambapo waweza kuchukua ibada nzima kwa moja ya haya, bali nataka kukomea hapa kwa muda mdogo kusisitiza hayo. Mwa—mwa—mwamini alipaswa kujitambulisha kwa sadaka yake. Mnaona? Kama ni sadaka tu na—na ilifanyiwa mahali fulani kule nje, aliitoa; bali alipaswa kujitambulisha katika hiyo. Hakika, ilimpasa kuweka mikono yake juu yake, kwanza, kujitambulisha mwenyewe na sadaka yake. Halafu hiyo damu iliwekwa mahali ambapo angeweza kusimama chini ya damu. Ile damu haina budi kuwa juu yake. Na hiyo ilikuwa ishara ya kwamba amejitambulisha, mwenye hatia, na kuthibitisha ya kwamba kitu kisicho na hatia tayari kimechukua mahali pake.

55 Ni picha nzuri jinsi gani! Lo, aliyekombolewa! Mnaona, haki ilikuwa imetimizwa, na masharti ya haki takatifu ya Mungu yalikuwa yametimizwa. Naye Mungu alisema, “Sasa nahitaji uhai wako,” kisha ule—ule—ule uhai ulikuwa umetenda dhambi. Basi kitu kisicho na hatia kikapachukua mahali pake. Na ilikuwa mnyama mwenye damu; si tofaa, tunda kama embe. Hiyo inapaswa kuufanya uzao wa nyoka dhahiri sana kwa kila mtu, ya kwamba ilikuwa ni damu. Na hii damu, ambayo haingalitoka kwenye tunda, ilitoka kwenye kitu kingine kisicho na hatia. Nao ule uhai ulikuwa umetoka, pia—pia, mahali pake, nayo hiyo damu ilikuwa alama ya kwamba huyo mnyama alikuwa amekufa na damu ikatoka.

56 Naye mwabudu alipojinyunyizia damu, alionyesha ya kwamba yeye alitambulikana katika ukombozi, kwa sababu amejitambulisha kwa . . . kwenye hiyo sadaka, akijiunganisha na sadaka hiyo, nayo ile damu iliwakilisha ile ishara.

57 Ajabu vi—vipi! Ni picha ya jinsi gani! Ni mfano mkamilifu wa Yesu Kristo, mkamilifu kabisa, mwamini leo akisimama chini ya Damu iliyomwagika, akijitambulisha na ile Sadaka. Ni kamilifu i—iwezavyo kuwa. Na jinsi Kristo, kwa kuwa ha—hakuwa mnyama. . .Mnaona, m—mnyama alikufa, bali alikuwa. . .

58 Kitu kisicho na hatia kabisa tulicho nacho, nadhani, kingekuwa m—mnyama, mwana—mwana-kondoo. Mungu alipotaka kumtambulisha Yesu Kristo, alimtambulisha kama Mwana-Kondoo. Naye alipotaka kujitambulisha Mwenyewe, alijitambulisha kama ndege, Hua. Naye hua ndiye ndege asiye na hatia hata kidogo aliye msafi sana miongoni mwa jamii yote ya ndege, naye mwa—mwana-kondoo ndiye asiye na hatia kabisa na msafi sana kati ya jamii yote ya wanyama. Kwa hivyo mnaona wakati. . .

59 Yesu alibatizwa na Yohana, na Biblia ilisema, "Naye—naye akamwona Roho wa Mungu, kama hua, akishuka juu Yake." Kwa hivyo kama ilikuwa. . .Kama ilikuwa mbwa mwitu, ama kama ingelikuwa mnyama mwingine ye yote, ile—ile tabia ya hua haingaliambatana na tabia ya mbwa mwitu, wala ta—tabia ya hua kuambatana na ya mnyama mwingine ye yote ila mwana-kondoo. Nazo hizo tabia mbili zikapatana, ndipo zingekubaliana moja kwa nyingine.

60 Basi sasa mnaona kuchaguliwa tangu awali? Alikuwa mwana-kondoo wakati alipokuja kule. Mnaona? Mnaona? Yule. . .Alikuwa mwana-kondoo alipo—alipotolewa. Alikuwa mwana-kondoo. Alizaliwa mwana-kondoo. Alilewa, mwana-kondoo. Mnaona?

61 Na, kwa hivyo, hiyo ndiyo tu Roho iliyo ya kweli inayoweza kupokea Neno, inayoweza kumpokea Kristo. Zingine zitajaribu, walijaribu kulipata, wakaweka Roho wa Mungu juu ya mbwa mwitu, mnaona, mwenye hasira, mwovu, duni. Hatadumu mle. Roho Mtakatifu huondoka papo hapo. Hatafanya hivyo.

62 Vipi kama huyo hua alishuka, na, badala ya kuwa Mwana-Kondoo, kungalikuwako mnyama mwingine? Angaliruka upesi na kurudi. Mnaona? Bali alipotaka ile tabia ambayo ingepatana naye, wakawa tu Mmoja.

63 Ndiposa yu—yu—yule Hua akamwongoza yule Mwana-Kondoo, na, tazama, alimwongoza yule Mwana-kondoo hata machinjioni. Basi, yule Mwana-Kondoo alimtii Hua. Mnaona? Haidhuru alikoongozwa, alikuwa tayari kwenda.

64 Nashangaa, leo, Mungu anapotuongoza kwenye ma—maisha ya kujitolea kabisa kwa utumishi Wake, nashangaa iwapo roho zetu wakati mwingine haziasi, hiyo ikionyesha dhahiri ya kwamba, nashangaa iwapo sisi ni wana-kondoo? Mnaona? Mnaona? Mwana-kondoo ni mtiifu.

65 Mwana-kondoo hujitolea kuwa sadaka mwenyewe. Yeye—yeye ha—hachukui, hadai vilivyo vyake. Unaweza kumlaza chini na kumkata manyoya. Hicho ndicho kitu pekee alicho nacho pekee. Ha—hasemi neno lolote; hutoa tu cho chote alicho nacho. Huyo ndiye mwana-kondoo. Hutoa kila kitu kwa . . . hutoa kila kitu, yeye mwenyewe na yote aliyo.

66 Hivyo ndivyo Mkristo halisi alivyo, kama wao . . . wanajitolea wenyewe, hawajali ya ulimwengu huu, bali wanatoa yote waliyo nayo kwa Mungu. Mnaona?

67 Na sasa huyu alikuwa Mwana-Kondoo mkamilifu, Kristo alikuwa hivyo. Kisha kupitia kwa ile iliyomwagika ya mwana-kondoo huyu, yule mwana-kondoo wa kawaida kule Misri, damu ilipakwa, kisha, ilipopakwa iliwakilisha ishara, basi, Damu ya huyu Mwana-Kondoo ingewakilisha nini? Mnaona? Ile Ishara ya kwamba tumekufa kwa nafsi zetu na tukajitambulisha na Sadaka yetu. Mnaona? Ndipo, yule Mwana-Kondoo na ile—ile—Damu na yule mtu wanatambulishwa pamoja, ile Sadaka na mwamini. Mnaona? Unatambulishwa maishani mwako, kwa sadaka yako. Hiyo inakufanya kile ulicho.

68 Wakati huo damu ilikuwa ishara, ama kitambulisho. Ile damu ilionyesha ya kwamba anayeabudu alikuwa amemchinja mwana-kondoo, na kumkubali huyo mwana-kondoo, na kujikupaka hiyo ishara yeye mwenyewekwamba yeye hakuona haya. Hakujali nani aliyeiona. Alitaka kila mtu aione, nayo ilikuwa mahali wazi kabisa hata kila mtu aliyepita karibu angeiona hiyo ishara.

69 Mnaona, watu wengi wanataka kuwa Wakristo, nao wa—wa—wanataka kufanya hivyo kwa siri kusudi mtu ye yote a—asipate kujua ya kwamba wao ni Wakristo. Ama, wa—wale wao wanaotembea pamoja nao, wengine wao wanafikiria, "Vema, tazama sasa, na—na nataka kuwa Mkristo, bali sitaki *fulani* ajue hayo." Mnaona? Vema, sasa, unaona, huo si Ukristo.

70 Ukristo unapaswa kuonyesha ishara yake, mnaona, hadharani, katika maisha ya umma, afisini, barabarani, kwenye shida, cho chote kile, kanisani, kila mahali. Damu ndiyo Ishara, nayo Ishara haina budi kuwekwa, mnaona, au (la sivyo) hata hilo agano halina maana.

71 Ile damu ilikuwa ishara, ama kitambulisho, ikionyesha ya kwamba mtu huyu amekwisha kukombolewa. Naam, vema, tazama, wao walikuwa, wao walikuwa wamekombolewa hata kabla hakijatendeka kitu cho chote. Kwa imani wao walipaka ile damu. Mnaona, kabla halijatendeka bado, ile damu ilipakwa kwa imani, wakiamini litatendeka. Mnaona? Kabla hasira ya Mungu haijapitia nchini, ile damu ilipaswa kupakwa, kwanza. Ilikuwa imechelewa sana baada ya ile ghadhabu kuanguka.

72 Naam, tuna somo hapo ambalo kweli tunaweza, labda kulileta mawazoni mwenu, kwa kitambo kidogo tu. Tazama,

*kabla* haijatendeka, kwa kuwa wakati unakuja ambapo hautaweza kupaka Damu yo yote.

73 Yule mwana-kondoo alivawa wakati wa jioni, baada ya kuwekwa kwa siku kumi na nne. Kisha huyo mwana-kondoo akauawa na damu ikapakwa wakati wa jioni. Mmeelewa hilo? Ile ishara haikuweko mpaka wakati wa jioni.

74 Na huu ni wakati wa jioni wa nyakati tunazoishi. Huu ni wakati wa jioni kwa—kwa Kanisa. Huu ni wakati wa jioni kwangu mimi. Huu ni wakati wa jioni wa Ujumbe wangu. Ninakufa. Mimi ninaenda. Ninaondoka, katika wakati wa jioni wa Injili. Nasi tumepitia katika kuhesabiwa haki, na kadhalika, bali huu ndio wakati ambapo ile Ishara haina budi kutiwa. Naliwaambieni Jumapili iliyopita nina jambo ningetaka kuwaambieni; ndilo hili hapa. Ni wakati ambao ha—hauwezi kuichezea. Haina budi kufanywa. Iwapo itafanywa kamwe, inapaswa kufanywa sasa. Kwa maana, tunaweza kuona ya kwamba hasira iko tayari kupitia juu ya uso wa nchi, na cho chote kisicho chini ya hiyo Ishara kitaangamia. Ile Damu, imekutambulisha. Tazama.

75 Kwa kuwa, uhai wa mnyama haungelimrudia mwanadamu. Damu ilipomwagika, uhai ulitoka, bila shaka, kwa maana vilikuwa kitu kimoja. Na wakati ule uhai wa hiyo damu ulipotoka kwayo, huo uhai ukiwa tofauti na hiyo damu . . . Naam, damu ni kemia ya uhai, bali uhai ni kitu tofauti na damu, bali uhai u katika damu. Nao huo uhai wa mnyama haungalimrudia anayeabudu. Alipomwaga hii damu ya mwana-kondoo, ilimpasa kupaka hiyo kemia, kwa sababu ule—ule uhai uliisha ondoka nao haungerudi.

76 Kwa maana, haungalimrudia mwanadamu, kwa maana uhai wa mnyama hauna nafsi. Mnyama hajui yeye yu uchi, naye—naye . . . Hatambui dhambi. Haijui kabisa, kwa hivyo basi ni kiumbe kilicho hai bali si nafsi iliyo hai. Kwa hivyo, huo uhai wa mnyama haungalimrudia katika maisha ya binadamu, kwa kuwa hapakuwamo na nafsi katika uhai huo. Sasa, kuna uhai, damu; uhai, na nafsi katika huo uhai; nafsi ndiyo tabia ya uhai. Kwa hivyo, hakuwa na tabia dhahiri, alikuwa mnyama, kwa hivyo ile damu ilikuwa ishara kwamba uhai umekwisha tolewa.

77 Bali katika mahali hapa penye utukufu, chini ya agano hili, kuna tofauti kati ya Damu na Uhai. Ishara kwa mwamini leo ni Roho Mtakatifu; si damu, kemia, bali ni Roho Mtakatifu wa Mungu. Hiyo ndiyo Ishara ambayo Mungu anayohitaji kwa Kanisa leo. Mungu hana budi kuiona hii Ishara. Hana budi kuiona katika kila mmoja wetu.

78 Kwa hivyo, vivuli vya jioni vinapojitokeza, na hasira iko tayari kushushwa kutoka Juu, juu ya mataifa yasiyomcha Mungu, na juu ya wasioamini wasiomcha Mungu, juu ya—ya wanaokiri wasio na chochote, juu ya mambo haya! Nami ni—

nimejaribu kujionyesha wazi na kuishi maisha mema miongoni mwake, kuona ilikokuwa imesimama, kabla sijasema mambo haya. Sasa tunaishi kwenye vivuli, nayo hasira iko karibu kushuka, naye Mungu anahitaji ile Ishara ya kwamba wewe binafsi umepokea Ishara Yake, Roho Mtakatifu. Ndiyo njia pekee, na ishara pekee ambayo Mungu atapita, kwa sababu ni Uhai halisi wa Yesu Kristo uliomrudia mwamini.

79 Uhai wa mnyama haukuweza kurudi, kwa hiyo damu ilipaswa kutiwa mlangoni, katika kizingiti na katika miimo ya mlango; kusudi kila mpitaji, watu wote, kila mtu anayepita karibu na hiyo nyumba, alijua ya kwamba kulikuwa i—ishara juu ya mlango huo, ya damu, ya kwamba uhai ulikuwa umekufa tayari hapo mlangoni. Amina!

80 Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa kwa kila mwamini leo, kujazwa na Roho Mtakatifu; Ishara ya kwamba Damu ya Mwana-Kondoo, ya kwamba ule Uhai uliokuwa katika yule Mwana-Kondoo, umekwisha kurudi na umetiwa muhuri ndani hapo, mbele ya watu wote, kusudi kila apitaye pale, anayezungumza na wewe, aliye na uhusiano wo wote nawe, ataona hiyo Damu imetiwa, na ile Ishara ya Uhai uliokuwa katika hiyo Damu uko juu yako. Hutapatwa na ile hasira. Ni hiyo pekee; si kuwa mshiriki. La, bwana!

81 Uhai wa mnyama haungalikuja juu ya mwamini, kwa sababu ilikuwa ni mnyama, nao ulinena kwa dhamiri, ukionyesha kuwa Sadaka kamilifu itakuja.

82 Na, sasa, kungewezaje kuwa na Sadaka kamilifu kuliko Mungu Mwenyewe akiwa Upatanisho, Yeye Binafsi? Mungu alipofanyika mwili, katika Damu Yake Mwenyewe inayoumba, hiyo ndiyo njia pekee ambayo Uhai wa Mungu ungaliweza kurudi.

83 Kwa maana, sisi sote tulizaliwa kwa kujuana kimwili, na kwa hivyo, uhai ulio mle ndani ni wa ulimwengu, na uhai huo hautadumu. Ni kitu ambacho tayari kimekwisha kuhukumiwa na kulaumiwa. Hauwezi kuutengeneza. Hautengenezeki. Hakuna njia ya ku—kuulainisha. Hauwezi kuwa bora. Hauna budi kufa! Hilo ndilo tu linalohitajika. Hauna budi kufa.

84 Na badala yake, Uzima wa Yesu Kristo, hauna budi kuingia ndani yako, ambao ni Roho Mtakatifu, Ishara ya Mungu; ya kwamba umeikubali Damu ya Mwanaye, Yesu Kristo.

85 Kwa hivyo, katika siku za Wesley ama . . . Siku za Luther, ilidhaniwa, "kuamini." Katika siku za Wesley, "kemia ya ile Damu." Bali hizi ni siku za mwisho, ambapo ile—ile Ishara inahitajika. Hiyo inaunganisha, pamoja, kitu hicho chote kwa ajili ya Kunyakuliwa. Mnaona? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

86 Maji, damu, na roho hutokea mama anapomzaa mtoto. Kitu cha kwanza kutokea, katika uzazi wa kawaida, ni maji, cha pili ni damu, kinachofuata ni uhai.

87 Kulitokea katika mwili wa Bwana Yesu Kristo: maji, Damu, na Uhai. Nalo Kanisa lote, Bibi-arusi, pamoja, wamefanyizwa kupitia kuhesabiwa haki, kutakaswa, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, ambao ndio ile Ishara.

88 Kama Waebrania 11 inavyosema, "Hawa wote walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na mbuzi, nao walikuwa wahitaji, na mambo haya yote waliyotenda, bali hawakukamilishwa pasipo sisi."

89 Na Kanisa siku hizi, ambalo limepokea ile Ishara, ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu, ya kwamba ile Damu imekwisha kumwagika, na ya kwamba Roho Mtakatifu yumo juu ya Kanisa; pasipo sisi, basi, hao hawawezi kufufuka. Bali wao wanatutegemea, kwa maana Mungu aliahidi atakuwa nayo, na mtu fulani atakuwa huko. Sijui atakuwa ni nani, bali mtu fulani atampokea. Nina jukumu moja tu, kuihubiri. Ni kazi ya Mungu kumtafuta huyo mzao aliyechaguliwa tangu awali. Watakuweko, hata hivyo. Kwa sababu, watakuweko, kila mmoja, wao wote pamoja; ule wakati wa maji, wakati wa damu, na sasa wakati wa ile Ishara ya Roho Mtakatifu.

90 Na, kumbukeni, Israel walipitia mambo mengi, bali ulikuwa wakati wa jioni ambapo ishara ilihitajika; si asubuhi, si katika yale matayarisho, ya zile siku kumi na nne za kumweka yule mwana-kondoo. Israel walijua kitu fulani kinakuja.

91 Luther alijua pia, Wesley pia, vivyo hivyo Finney, Knox, Calvin, walijua. Ndicho hiki! Walijua wakati unakuja ambapo ile Nguzo ya Moto ingerudi Kanisani. Walijua wakati unakuja ambapo mambo haya yangetendeka, bali hawakuishi kuyaona, bali waliyatarajia.

92 Israel walijua jambo fulani lingetendeka, bali ilikuwa wakati wa jioni ambapo damu ya mwana-kondoo, ile ishara, iliwekwa mlangoni. Hata hivyo, mwana-kondoo alikuwa tayari ametolewa.

93 Amekuwa Mwana-Kondoo kila wakati. Alikuwa Mwana-Kondoo wakati wa Luther; Alikuwa Mwana—Mwana-Kondoo wakati wa Wesley, bali sasa ni wakati wa ile Ishara ambapo kila nyumba haina budi kufunikwa kwa ile Ishara. Kila nyumba ya Mungu haina budi kufunikwa kwa ile Ishara. Wote walio ndani yake hawana budi kufunikwa kwa hiyo Ishara. Nayo Nyumba ya Mungu ndiyo Mwili wa Yesu Kristo, na kwa Roho Mmoja sote tumebatizwa katika Ishara hii tukawa sehemu Yake, ambayo, Mungu alisema, "Nitakapoiona Ishara hii imewekwa, nitapita juu yenu." Ni wakati wa jinsi gani tunamoishi sasa! Lo!

94 Damu ilimtambulisha, ilimtambulisha mwamini, kwa maana ule uhai uliokuwa umetoka, haungerudi, kwa hivyo

ilimpasa kuwa na—na kemia. Ilimpasa kuwa nayo kama rangi, damu, kemia ilionyesha ya kwamba uhai tayari umetoka humo.

95 Sasa Roho Mtakatifu Mwenyewe ndiye Ishara. Roho Mtakatifu Mwenyewe ndiye Ishara, si Damu. Damu ilimwagwa Kalvari, hiyo ni kweli. Bali ile Damu, jinsi ilivyo, ilirudi kwenye vitu ilivyotoka kwake, kutoka katika chakula alichokula. Lakini, mnaona, ndani ya hiyo chembechembe ya damu kulikuwemo Uhai uliofanya hiyo chembechembe ya damu kufanya kazi. Kama ilikuwa. . . Ile Kemia haikuwa na uhai ndani yake, yenyewe, na kwa hivyo haingetenda kazi. Bali Uhai ulipoingia katika ile kemia ya damu, ukaumba chembechembe. Ukajitengenezea chembechembe Yake Wenyewe, kisha chembechembe baada ya chembechembe, ndiposa ikawa Mtu. Naye huyo Mtu alikuwa Mungu, Imanueli, katika mwili. Bali uhai huo uliporudi, ile kemia ikaingia mle, bali ile Ishara ni Roho Mtakatifu juu ya Kanisa, wapate kumwona Kristo.

96 Haina budi kuwa hivyo, kwa maana mwanamke na mumewe huwa mmoja. Wao huwa mmoja. Vivyo hivyo Bibi-arusi na Kristo watakuwa Mmoja. Huduma ya Bibi-arusi na huduma ya Kristo ni sawa. Na kumbukeni, "Kitabu kile cha kwanza, Ee Theofilo, nilichokuandikia, mambo aliyoanza Yesu kufanya na anaendelea kufanya." Kifo Chake hakikumkatiza. La, bwana! Yeye alirudi tena. Si nafsi ya tatu, bali Nafsi ile ile ilirudi tena katika mfano wa Roho Mtakatifu, na kuendelea kufanya kazi; na anaendelea mbele, kasema Kitabu cha Matendo. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Hiyo ndiyo Ishara. Hiyo ndiyo dalili.

97 Petro na Yohana walipopitia kwenye mlango uitwao Mzuri, palikuwa na mtu aliyekuwa kiwete, kilema toka tumboni mwa mamaye, naye akasema, "Mimi sina fedha, wala dhahabu; lakini nilicho nacho, ndicho nikupacho. Kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareth, simama uende." Mnaona? Nao wakazungumza nao na kujua ya kwamba walikuwa watu wasio na elimu, wasio na maarifa, bali waliwatambua ya kwamba walikuwa pamoja na Yesu. Waona, ile Ishara ilikuwa pale, ikionyeshwa. Mnaona, "Nilicho nacho!" Walipoona maskini ndugu alieyeanguka amelala pale, kiwete, ameumbuka, na kila kitu. Na uhai ule ule uliokuwa katika Kristo ulikuwa ndani yao, "Nilicho nacho!"

98 "Katika Jina Langu, mtatoa pepo." Si, "Mimi nitatoa!" "Ninyi mtatoa!" "Kama wewe ukiuambia mlima huu!" Si "Kama Mimi nikiuambia." "Kama wewe ukiuambia mlima huu!"

99 Lo, ndugu, saa ambayo hiyo Ishara haina budi kuonyeshwa waziwazi imewadia. Tunaweza kuiona. Tunajua tumekaribia mwisho sasa. Tumeleta kila namna ya jumbe, ishara na maajabu, na sasa hapa tunarudia yale Kanisa linapaswa kufanya. Ile Ishara haina budi kuonyeshwa. "Nitakapoiona Damu, nitapita juu yenu." Hamna kingine kitakachofaa. Hapana budi iwe

Damu. Sasa, Roho Mtakatifu ndiye Ishara yetu kutoka kwa Mungu.

100 Kama vile yule mwanatheologia mkuu, mwa—mwanachuoni, Ndugu Mbatisti, mtu mzuri, mwenye tabia nzuri, alivyonijia wakati mmoja, naye akasema, "Ndugu Branham," akasema, "unanena kuhusu huyu Roho Mtakatifu," kasema, "kwani, hilo si jambo jipya." Kasema, "Tumefundisha hayo daima, nyakati zote." Nami ni—nikasema, vema, nita . . . Akasema, "Tulimpokea Roho Mtakatifu."

101 Nikasema, "Ulimpokea lini?"

102 Akasema, "Nilipoamini." Maana, nilijua hiyo ni theologia ya Kibatisti, kwamba, "Wewe, unapoamini, unampokea Roho Mtakatifu."

103 Nikasema, "Basi Paulo alisema, katika Matendo 19, kwa kundi, kundi la Wabatisti, ambao, mhubiri Mbatisti aliyekuwa mmoja wa waongofu wa Yohana, alikuwa akithibitisha kwa Biblia ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo."

104 "Akiisha kupita kati ya pwani za juu za Efeso, akakutana na wanafunzi kadha wa kadha, akawauliza, 'Je! mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?' Wao wakasema, 'Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu." Kisha akawauliza jinsi walivyobatizwa. Nao hawakuwa wamebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, yule Mwana-Kondoo wa sadaka. Hawakuwa wamejitambulisha Naye, hata kidogo. Waliamini tu; kama dawa iliyo pale, nao hawakuwa wameinywa. Paulo akawaagiza wabatizwe tena, katika Jina la Yesu Kristo.

105 Na alipofanya hili, basi ile Ishara ikaja juu yao. Nao walitambulishwa kwa zile kazi na ishara za Roho Mtakatifu, akinena kwa lugha kupitia kwao, na kutabiri, na kumtukuza Mungu. Wao walijitambulisha kama—kama na Sadaka yao.

106 Na Roho Mtakatifu ndiye kitambulisho chetu. Ndiye anayetutambulisha kama Wakristo. Si ushirika wetu kanisani, si ufahamu wetu wa Biblia, si jinsi unavyoijua Biblia. Ni jinsi unavyomjua Mwandishi wake, unaona, ama jinsi huyo Mwandishi anavyoishi ndani yako. Ni—ni utu wako ukisha ondoka. Hauko tena . . . Unajihesabu umekufa, nayo ile Ishara ndiyo inayoishi ndani yako. Na si uhai wako; ni Yeye.

107 Paulo alisema, "Uhai nilio nao sasa." Yeye aliishi maisha tofauti na yale aliyoishi wakati mmoja. "Si mimi, bali Kristo ndani yangu." Ipo hapo Ishara iliyotambulishwa ambayo Mungu alihitaji. Kutambilishwa na . . . Utambulisho na Sadaka yetu, Uhai wa Mwokozi wetu ndani yetu, Roho Mtakatifu.

108 Lo, ni—ni Ishara dhahiri namna gani! Hapawezi kuwepo na Ishara nyingine. Jamani, laiti ungalipata wa—wazo lake. Laiti ningalikuwa na u—uwezo asubuhi hii, pamoja na maneno, kulieleza na kuliweka katika nafsi yako iliyo ndani; sio maskioni

mwako, bali nafsini mwako, nawe—nawe ungeliona dhamana yake. Ina—inachukua, inakufanya ustarehe kweli kweli.

109 Vipi kama ulikuwa, ulikuwa umevunja sheria, nawe unaenda kushtakiwa mahakamani. Nawe unajua, ya kwamba kama ulipatikana na hatia, kwamba ungeuawa, ungepelekwa kwenye kiti cha stima, au chumba cha hewa ya sumu, ama mauaji yo yote ya hadhara ambayo wangalikufanyia, labda unyongwe, ama cho chote kile, kuuawa kwa hasira, adhabu yo yote ile. Nawe ulijua ya kwamba ulikuwa. . . Ulikuwa na hatia. Unajua ulikuwa na hatia, nawe huna budi kufa usipompata wakili wa kukuwakilisha, anayeweza kukuondoa katika jambo hilo. Na sasa ungetaka wakili mzuri sana ambaye ungalimpata.

110 Ndiposa kumpata wakili mzuri hivyo, aliye mwerevu, ungejisikia ya kwamba kesi yako ilikuwa kidogo. . . ungepumua kidogo, kwa maana, ulikuwa na wakili. Basi hata hivyo kungalikuweko na swali, kama huyu wakili angalibadilisha wazo la hakimu ama abadilishe lile baraza la mawakili; iwapo huyu wakili, kwa maneno yake ya busara na ujuzi wa sheria angalibadilisha hayo, naye angalikutetea na kuthibitisha kwamba kwamba unapaswa kuishi. Lakini hata hivyo, mbali na uwezo wa—wake mkuu na matamshi yake makuu angaliweza kuyafanya, ushawishi angalikuwa nao juu ya hilo baraza la mawakili ama juu ya hakimu, wewe—unge—unge. . . Labda ungepumua kwa dakika chache, hata hivyo kungelikuwa na swali akilini mwako: “Je, atafaulu?”

111 Bali katika kesi hii, Hakimu Mwenyewe ndiye Wakili wetu. Mungu alifanyika mtu. Hamna wakili angaliweza kufanya hivyo. Hatungempata hata mmoja. Musa, na Torati, manabii, hamna angaliweza. Kwa hivyo Hakimu akawa wote pamoja Baraza la Mawakili, Wakili, na Hakimu, Mwenyewe; naye akatwaa haki ya Sheria Zake mikononi Mwake, kisha akalipa gharama yake, Yeye Mwenyewe. Tunawezaje kuwa salama zaidi? Naye akautuma Uhai Wake juu yetu, kama ushahidi ya kwamba Yeye ameikubali. Jinsi tulivyo salama!

112 “Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe upo pamoja nami.”

113 Alipofanyika vyote viwili Hakimu, Baraza la Mawakili, na—na Wakili, Yeye alitutetea. Sisi, tuliopatikana na hatia kwa Sheria Zake Mwenyewe; naye akaja na kupachukua mahali pa mtu mwenye hatia, hiyo ilikuwa katika mahali patakatifu. Alichukua dhambi yake. Alizibeba nafsini Mwake, na alikufa, na kulipa ile gharama, alimwaga damu Yake, kisha alitoa Ishara Yake Mwenyewe, Uhai Wake.

114 Kwani, sisi tu wakamilifu. Kesi imeondolewa. Hamna tena dhambi kwa mwamini. Ee Mungu, uturehemu, ikiwa watu hawawezi kuona hayo, ya kwamba kesi haipo tena. “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka,

yuna Uzima wa Milele, naye hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ndiyo hiyo kesi hapo. Kesi imeondolewa! Hamna mashtaka tena. Amina! Basi tu salama, tu salama huku ile Ishara imepakwa, wakati mauti yatakapoanza kupiga-piga mlango huko nje, hayawezi kututawala. Mnaona? Ndio.

115 Ile Ishara imekwisha kupakwa. Hiyo Ishara ndiyo pekee inayotambuliwa sasa. Mnaona, Yeye alifanya hivyo kusudi ile Ishara ipate kuja. Ishara ilikuwa Uhai wa Mungu.

116 Kisha Mungu alipomfanya mtu wa kwanza, alimfanya mwana. Naye huyo mwana alikuwa mpotevu sana hata akamsikiza mkewe, badala ya Mungu, naye huyo mwanamke akamsikiliza ibilisi badala ya mumewe, halafu, hiyo ilipotendeka, ikawapotosha sana wote pamoja, hata ikasababisha unajisi. Naye alijua, ya kwamba wao walipofanya hivyo, itawabidi kuwaleta watoto ulimwenguni. Lile tunda katikati ya mti halingaliguswa, ndipo, basi, lilipoguswa, wakajiletea dhambi juu yao. Hivyo basi, jamii yote ya mwanadamu iliyozaliwa, ilikuwa katika dhambi. Pale, hamna njia ya kutokea.

117 Ndiposa, Mungu akashuka. Kuna njia moja tu ya kumrudisha; hiyo ni kumfanya mwana tena. Naye anawezaje kufanya hivyo, huku Sheria Yake ilisimama pale ikisema "amekwisha hukumiwa"? Kisha Baba Mwenyewe akawa mmoja wetu. Huyo ndiye Mwana-Kondoo halisi. Hilo ndilo kusudi alilokuwa nalo niani.

118 Hiyo ndiyo sababu Mwana-Kondoo alitambulishwa kabisa katika Bustani ya Edeni, akijua ya kwamba Mwana-Kondoo pamoja na Hua wangalikutana wakati mmoja, ambapo Mwana-Kondoo na Hua wangekuwa pamoja. Hapo ndipo alipojua, kupitia kwa hayo, sote tunaweza kuwa pamoja. Naye alikuwa tayari kufanya toleo kama hilo, sasa, kusudi ile Ishara ipate kupakwa, ya kwamba sisi si wapitaji tena, sisi si wageni tena, bali sisi ni wana na binti za Mungu. Wote wawili Adamu na Hawa, mwanamke na mwanamume, wakiungana pamoja, ni wana na binti za Mungu, katika Kristo Yesu, kwa lile toleo Lake kuu

119 Na, basi, ili kusiwe na kosa lo lote! Ile mbegu ya maisha haya ambayo haina budi kupandwa duniani, ya mwili huu ni—ni mbegu iharibikayo; na ule uhai, kama ni uhai uliopotoshwa katika mbegu unaangamia pamoja na hiyo mbegu. Bali Yeye aliweka Uzima wa Milele ndani yake na kuutambua kama ni Wake, Mwenyewe, ili kwamba katika ule ufufuo, Yeye angeufufua tena, haitapotea. Mnaona ninayomaanisha? [Kusanyiko laitikia, "Amina."—Mh.]

120 Ndio huo, hauwezi kuangamia sasa. Ule Uhai hukaa juu yake. Ni Ishara, hukaa juu ya huo mwili mdogo, hukaa juu

ya nafsi ya mtu huyo. Kuna Ishara kule, Roho Mtakatifu, ya kwamba ni mali ya Mungu. Ni Yake. “Nitakapoiona Ishara, nitapita juu yenu.” Ishara thabiti, Roho Mtakatifu ndiye Ishara yetu. Kwa hiyo, unapompokea Roho Mtakatifu, unapita kutoka mautini kuingia Uzimani. Ni hayo tu, kwa maana Uhai umo ndani yako. Hauwezi kuangamia kamwe.

121 Biblia ilisema, “Kila mtu aliyezaliwa na Mungu, hatendi dhambi, kwa maana hawezi kutenda dhambi, kwa sababu Uzao wa Mungu,” amina, “Uzao wa Mungu wakaa ndani yake.” Basi anawezaje kutenda dhambi, na huku Mungu asiye na dhambi yumo ndani yake? Akiwa katika Mungu asiye na dhambi, awezaje kutenda dhambi? Haidhuru ametenda nini, Damu inamfunika. Mnaona? Yeye ni kiumbe kipya sasa. Shauku zake na tamaa zake ni za Mbinguni, kwa maana amebadilika kutoka gugu akawa ngano. Tamaa zake haziko tena kama zilivyokuwa hapo mwanzo, naye anaonyesha.

122 Unasema, “Lo, naamini hilo.” Na ungali unatenda dhambi? Jamani! Umedanganywa. Mnaona? Haiwezi kuonyesha kitu ila Ishara.

123 Israel waliamriwa kukaa chini ya ile damu hata amri ya kuanza safari ilipotolewa. “Msitoke chini yake.” Mara walipokuwa chini ya hiyo ishara, walitiliwa muhuri mle. “Msiiache!” Walikaa pale pale, hata usiku wa manane ulipofika, na tarumbeta zikalia. Nazo tarumbeta zilipolia, na maskini zile pembe za kondoo dume zikaanza kulia, kila mtu alitoka pamoja na masurufu yake, akielekea kwenye nchi ya ahadi.

124 Vivyo hivyo na mwanamke na mwanamume aliyejazwa Roho Mtakatifu, yeye ametiwa muhuri na yu salama tokana na madhara yote na hatari. Maisha yake yote yanaonyesha alivyo yeye, po pote aendapo, kazi yo yote afanyayo, ye yote anayezungumza naye. Anapokutana na wanawake, anapokutana na wenziwe, anapokutana na kila kitu, ile Ishara iko mle. Amina! Anapofika mautini, “Sitaogopa mabaya; kwa maana Wewe upo pamoja nami,” hiyo Ishara inakaa pale. Inapokuja kwenye ufufuo, atakuwepo, kwa maana Mungu atamfufua katika siku ya mwisho. Yesu alisema hivyo! “Nitakapoiona damu, ile Ishara, nitapita juu yenu.” Lo!

125 Kumbukeni, kama hiyo Ishara haikuonyeshwa dhahiri, hata lile agano lilitanguliwa. Hiyo ni kweli. Agano lilitanguliwa. Hapakuweko—hapakuwepo na agano mradi tu hiyo Ishara haikuweko. Ishara ilikuwa badala ya agano. Mungu alifanya agano pamoja nao, naam, bwana. Bali Ishara ilipaswa kuwepo. Halikutumika, agano halikutumika, isipokuwa Ishara iwepo.

126 Huenda Wayahudi wengi wangesema, “Njoo hapa, sina damu yo yote mlangoni mwangu, bali nataka kukuonyesha kitu fulani, mimi ni Myahudi aliyetahiriwa. Nimetahiriwa.” Hiyo

haikumaanisha *hivyo*. [Ndugu Branham adata kidole chake.—Mh.] "Nitakapoiona Damu! Nitakapoiona Ishara."

127 Huenda ukasema, "Mimi ni Mbatisti, Mpresbeteri, Mmethodisti," ama cho chote unachotaka kuwa."

Bali, "Nitakapoiona ile Ishara!"

128 Unasema, "Mimi ni mwamini. Mamangu alikuwa mfuasi wa kanisa hili. Babangu alikuwa mfuasi wa kanisa hili. Nimekuwa mfuasi kule tangu utotoni." Hiyo haimaanishi *hivyo*. [Ndugu Branham adata vidole vyake]. "Sisemi uongo, siibi, sijafanya *hii*. Mimi . . ." Hayo hayamaanishi *hivyo*. [Ndugu Branham adata vidole vyake—Mh.] "Mimi ni mfuasi wa Maskani ya Branham. Nafanya *hili, lile* au *linginelo*. Neno lote."

Hao Wayahudi wangesema, "Namwamini Yehova!"

129 Ungalisikiza Ujumbe wa wakati huo, kama ulimwamini. Bila shaka. Wao walikuwa wamepata jumbe nyingi sana, bali huu ulikuwa ndio Ujumbe wa wakati huo. Mnaona? Naamini Ujumbe wa wakati huu. Naam, damu ilitiwa wakati wa jioni.

Huenda wao walisema, "Mimi, mimi ni Myahudi."

130 Watu husema leo, "Mimi ni Mkristo. Naweza kukuonyesha ushirika wangu wa muda mrefu. Nakutaka uniambie po pote nilipoiba cho chote, nikapata kuwa mahakamani. Nionyeshe nilipopata kufanya uzinzi. Sijafanya mambo haya yote, ama kitu kama hicho. Nionyeshe mahali pamoja." Hilo halimaanishi cho chote sasa. La, la. Mnaona, haidhuru alikuwa wa agano jinsi gani, hilo agano halikutumika. Halifai kitu.

Unasema, "Vema, mimi ni mwanafunzi wa Biblia."

131 Sijali wewe u nini. Pasipo hilo agano, hasira ya Mungu inakukalia. Unaona? Sawa. Imekushika. Naam. "Dhambi zako zitakupata." Dhambi ni nini? Kutokuamini. Huamini Ujumbe. Huamini Neno. Huamini ushuhuda wa Ishara, Yenyewe, inapojitambulisha kati yetu. Nawe umekataa kuamini Hiyo? Haidhuru utakosa kuamini vipi, haina budi kupakwa.

132 Huenda ukasema, "Naamini. Naamini. Naamini ni Kweli. Nakubali ni Kweli." Basi hayo yote ni mazuri, bali hata hivyo haina budi kuwekwa.

133 Naam, huyu Myahudi akisimama pale, akikoroga-koroga damu, huku mwana-kondoo anatokwa na damu, akisema, "Huyu ni Yehova,"

134 Naye kuhani alisimama pale, akisema, "Naam, bwana, naamini hiyo ni kweli," lakini nyumbani kwake mwenyewe, haijatiwa bado. Hataki kujitambulisha mwenyewe kule nje na hilo kundi; la, bwana, hawa washupavu wa dini wenye damu milangoni. Hataki utambulisho huo. Haidhuru alikuwa kuhani vipi, alijua Neno vipi, walimlea vizuri jinsi gani, alikuwa

amefanya kazi gani, alikuwa ametoa vipi kwa maskini, alikuwa ametoa sadaka vipi!

135 Paulo alisema, "Nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama dhabihu; nitoe mali zangu zote kuwalisha maskini; niwe na imani ya kuhamisha milima, na kadhalika; na kunena kwa lugha, kama wanadamu na malaika; na mambo haya mengine yote," na akasema, "Si kitu mimi mpaka ile Ishara imekwisha pakwa. Hata hii Ishara!" Hayo ndiyo ninayonena habari zake usiku wa leo, upendo. "Naam, hadi hii itakapopakwa, si kitu mimi." Mnaona?

136 Sijali, huenda ikawa ulitoa pepo, huenda ikawa uliwaponya wagonjwa kwa maombi yako ya imani. Huenda ikawa ulitenda mambo haya yote. Basi iwapo hiyo Ishara haipo, wewe uko chini ya hasira ya Mungu. Huenda ikawa u mwamini. Huenda ukasimama mimbarani ukahubiri Injili. "Wengi watakuja Kwangu siku hiyo, waseme, 'Bwana, Bwana, je, sikutoa unabii katika Jina Lako, nikahubiri katika Jina Lako? Je, sijatoa pepo katika Jina Lako?" Hao ni wote pamoja Wamethodisti, Wabatisti na Wapentekoste. Yesu alisema, "Ondokeni Kwangu, ninyi nyote mtendao maovu. Sikuwajua ninyi kamwe."

137 "Bali nitakapoiona Ishara, nitapita juu yenu." Ndiyo masharti ya Mungu ya wakati huu. Ujumbe wa wakati wa jioni, ni kupaka Ishara.

138 Shetani amewatupia namna zote za maigizo, ya kupeana mikono na madhihirisho, na kila kitu hivyo. Sahau! Wakati umewadia ambapo ni Ishara, Yenyewe; si maigizo fulani, kujifanya kuamini vibadilisho, cho chote kile.

139 Wakati umewadia ambapo Ishara Mwenyewe anajitambulisha mumu humu miongoni mwetu, na kuthibitisha ya kwamba Yeye ndiye Yesu yeye yule jana, leo, na hata milele, naye yu pamoja na Neno. Haina budi kupakwa. Mtu anayesema kwamba ana Ishara, na anakana hili Neno, vipi basi? Hauwezi kufanya hivyo. Ishara haina budi kuweko. Nitakapoi . . . Damu itakuwa Ishara kwenu." Sasa, Roho Mtakatifu, ule Uhai uliokuwemo katika ile Damu, ndiyo Ishara kwenu. Iendeeni mara moja, mnaona. Roho Mtakatifu ndiye ile Ishara. Kesi imekwisha. Naam, bwana. Sasa, kumbukeni. Nami . . .

140 Haidhuru wewe u nini, u mwema vipi, umeruka *juu-chini* mara ngapi, umejiunga na makanisa mangapi, umefanya mambo mazuri mangapi; haitakufaa kitu iwapo ile Ishara haijapakwa. Huu ni wakati wa jioni. Hayo yalikuwa sawa katika siku za Luther, hayo yalikuwa sawa katika siku za Wesley, lakini hayafai sasa. La.

141 Naam, kumuweka yule mwana-kondoo ilikuwa sawa, wakati huo. Wale waliokufa wakati huo kabla mwana-kondoo huyo hajatumiwa, damu, ilikuwa kitu kingine tofauti. Naam, bwana.

Wao waliendelea kwa sababu ya dhamiri njema. Watahukumiwa kana kwamba wao—wao walikuwa . . .

142 Kama walichaguliwa tangu awali, iliwagusa. La sivyo, haiwagusi. Hivyo tu. Ni Mungu tu. Yeye—Yeye huhesabia haki yule atakaye, humrehemu yeye amrehemuye, naye humhukumu atakaye mhukumi." Yeye ni Mungu. Hivyo tu. Humrehemu yeye amrehemuye, na kumhukumu anayetaka kumhukumu."

143 Myahudi angeonyesha waziwazi, kwa tohara, ya kwamba yeye ni mwamini.

144 Kuna watu wengi, watu wa kiasili, wanaoweza kuchukua Biblia hii na kusema, "Mimi ni mwamini, naye Yesu alisema 'kwa imani' tumeokolewa. Pia mimi ni mwamini, bali huo ubatizo wa Roho Mtakatifu ni upuzi." Basi Ishara haijapakwa. Si hoja, haidhuru anaamini vipi, imetanguliwa.

145 Ni kama tu ile tohara ya Myahudi. Yeye alisema, "Mimi ni Myahudi. Mbona, mbona niende kule na kutenda kama kundi lile lingine la washupavu wa dini?"

146 Musa akisimama, huku na huko barabarani, akisema, "Ujumbe wa jioni uko hapa! Itakuwa ya kwamba, siku kumi na nne zitakapokwisha, mtakusanya kusanyiko pamoja na kumchinja mwana-kondoo. Kusanyiko lote la Israel watamchinja, wakiweka mikono yao juu yake, wakijitambulisha naye. Nayo damu itatiwa kwenye miimo, na kwenye vizingiti vya mlango, nami 'Nitakapoiona damu, nitapita juu yenu, kwa kuwa ni ishara ya kwamba mmekubali kifo cha mwana-kondoo niliyewapa ninyi?'" Damu ilikuwa ishara.

147 Sasa Roho ndiye Ishara. "Mtajazwa na Roho Mtakatifu baada ya siku chache." Nayo Damu ilipomwagika, Ishara ikashushwa kwenye siku ya Pentekoste, kama upepo wa nguvu ukienda kasi.

148 Hicho ndicho kilikuwa kiini cha kila mtume. Hiyo ilikuwa, "Je, mmepokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?" "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa hiki cha Roho Mtakatifu, kwa maana ndiyo Ishara, amina, ya kwamba mmepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Ndivyo hivyo. Wakati hilo la Matai . . . Kanisa la Kiyahudi lilipotoweka, Mataifa yalichukua mahali pake, na huo upotovu hivyo; sasa limetokea, lipate kuchukua hayo masalio ya Mataifa, kwa ajili ya Jina Lake, Bibi-arusi.

149 Mnaona yale ninamaanisha? Mnaona yale Maandiko yanazungumzia hapa? Kama Ishara haikuonyeshwa, basi lile agano halikufaa. Mnaona? Haina budi kuwa hivyo. Maana, kama ukisema unaamini, nawe huyafuati maagizo ya Neno, basi huamini. Unaona? Hata ikiwa umetahiriwa, hata ukijiunga, na hata kama umebatizwa, umetenda mambo haya yote hivyo; hiyo bado siyo ishara, Roho Mtakatifu.

150 Huyu mwanachuoni bora akaendelea kunena nami, kama nilivyosema muda mchache uliopita. Akasema, “Billy,” akasema, “Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki. Mtu huyo angefanyaje zaidi ila kuamini hayo?”

151 Nikasema, “Hiyo ni kweli, Daktari. Ni kweli Yeye alimwamini Mungu. Biblia ilisema hivyo. Umesema kweli. Umbali uliofikia, umesema kweli.”

152 Mradi tu wale wa—wa—wapelelezi kumi na wawili, waliotumwa kwenda kuipeleleza nchi ya Kanaani, mradi tu walikuwa wakielekea Kanaani, walikuwa wakiendelea mbele; bali walipofika mpakani, basi wakakataa.

153 Nikasema, “Ninyi Wabatisti mko sawa, umbali mliofikia, bali je, mmepokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?” Nikasema, “Kumbukeni, Mungu aliitambua imani ya Ibrahimu. Ye—Yeye alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki. Hiyo ni kweli, hata hivyo Mungu alimpa muhuri wa tohara, kama ishara, ishara kwake.” Si eti mwili wake, uliotahiriwa, ulikuwa na uhusiano wo wote na nafsi yake, bali ilikuwa ishara kwamba (Mungu aliisha) itambua imani yake.

154 Naye hutupa sisi ishara, ya Roho Mtakatifu, ya kwamba Yeye ametutambua kama waamini. Kwa kuwa, “Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu katika Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu!”

155 Mnafahamu sasa. Hao Wayahudi, haidhuru wangethibitisha mara ngapi ya kwamba walikuwa wametahiriwa, hata hivyo ishara ilipaswa kuonyeshwa. La sivyo, lile agano halikufaa. Halikufaa.

156 Vivyo hivyo sasa, jambo lile lile. Haidhuru utafanyaje, haidhuru unaweza—unaweza kuifafanua Biblia vipi. Huenda ukawa mwanafunzi wa Biblia. Lo, jamani! Huenda—huenda ukasema, “Mimi ni mwamini, na kila kitu.” Hata hivyo Ishara inahitajika. Mwanafunzi wa Biblia, unasema, “Nilikuwa mtu mzuri, Ndugu Branham.”

157 “Sijali asemayo mtu ye yote, hauwezi ukamshinda mtu huyo. Sijamwona kamwe akitenda jambo lisilofaa, maishani mwangu.” Hilo halina uhusiano *huo* na Mungu [Ndugu Branham an vidole vyake]. Kuna sharti moja, na hilo pekee!

158 Nawe hauwezi kufanya hivyo. Huwezi kutia damu kwenye kizingiti cha mlango, ambapo, ishara haingalikuwepo isipokuwa mwana-kondoo amekufa. Nayo ile damu ilikuwa ishara thabiti ya kwamba mwana-kondoo alikufa. Si hila; mwana-kondoo alikufa.

159 Roho Mtakatifu ni Ishara thabiti ya kwamba Mwana-Kondoo wako alikufa nawe ukapokea Ishara nafsini mwako, maana uhai Wake hasa umo ndani yako. Unaona? Hamna hila.

Hamna kujifanya. Hamna kuigiza. Ipo! Unajua hivyo. Unajua hivyo. Ulimwengu unajua. Ishara iko.

160 Haidhuru mtu huyo alikuwa mzuri vipi. Huenda ikawa alikuwa mwanafunzi wa Biblia. Huenda ikawa. . . Huenda ikawa namna yo yote ya—ya mshiriki mzuri wa kanisa. Huenda ikawa ni mtu mzuri. Huenda ikawa ni kiongozi wa dhehebu fulani. Labda ni ukasisi wa Rumi. Si—sijui ni nani, si—haifai kitu.

161 Bali, Israel, mwanafunzi ye yote wa Biblia anajua ya kwamba Israel walikuwa mfano wa Kanisa, bila shaka, wakienda kwenye nchi ya ahadi. Na huko ndiko anakoelekea.

162 Bali wakati wa jioni ulipowadia, na safari ilikuwa imeanza, kulikuwa na sharti moja muhimu. Haidhuru alikuwa Myahudi vipi, jinsi alivyokuwa ameilinda mimea yake vizuri, jinsi alivyokuwa amewasaidia jirani zake, jinsi alivyokuwa ametenda mengi, jinsi alivyokuwa mshiriki mzuri, jinsi alivyokuwa ametoa fungu la kumi sana. Mambo hayo yote yalikuwa sawa. Hiyo ilikuwa sawa. Alikuwa mtu mzuri, ametambulikana kati ya watu wake, kama mtu mzuri. Bali bila ile ishara, ya damu, aliangamia.

163 Lo, Mungu na anisaidie, kwa wale walio humu na kwenye kanda, kusisitiza hilo!

164 Haidhuru, huenda ikawa ulihubiri Injili, huenda ikawa ulitoa pepo, huenda ikawa ulinena kwa lugha, huenda ikawa ulipaza sauti, ukacheza katika Roho, bali bila Ishara.

Unasema, "Je, naweza kufanya hivyo?"

165 Paulo alisema ungeweza. "Nijaposema kwa lugha kama wanadamu na malaika, nijapotoa mali yangu yote kuwalisha maskini, mwili wangu niungue moto kama dhabihu, nina imani kiasi cha kuweza kuhamisha milima, na mambo haya, si kitu mimi bado." Usitegemee hayo. Ni Ishara! Hata kama umetenda mengi vipi, u mwema jinsi gani; hasira ya Mungu itakaposhuka ghafla, itatambua tu Ishara.

166 Ni Ishara kwamba gharama imelipwa, ambayo ilihitajika. Na gharama iliyolipwa ilikuwa ule Uhai wa Yesu Kristo, naye alitoa Uhai Wake. Kisha Roho Wake akarudi juu yako, kama Ishara ya kwamba umepokewa. Na unaibeba Ishara nafsini mwako, usiku na mchana, si Jumapili tu. Ni wakati wote, una Ishara. "Wakati mimi . . . Ile damu itakuwa ishara kwenu."

167 Unasema, "Ningali ninaamini. Mimi ni mwamini." Hilo ni sawa. Bali ukikataa Ishara, basi utakuwaje mwamini? Inakupinga. Unaona, inapinga ushuhuda wako, ya kwamba unaamini.

168 Mwanafunzi wa Biblia, mtu mzuri, mshiriki wa kanisa, hata uwe nani, haifai kitu. Naam, bwana. Labda babako ni mhubiri. Labda mama ya—yako alikuwa mtakatifu. Labda. . .

Hiyo—hiyo ni sawa, hawana budi kujitetea wao wenyewe. Kama nilivyosema, jaribu . . .

169 Watu wengi hujaribu kumfanya Mungu maskini babu mnene na mnono wa kale aliyepungukiwa na akili, mnaona, mwenye vijukuu kadhaa, kama tu akina Ricky na Elvis wadogo, na, "Hao hawana madhara."

170 Si Mungu! Yeye hana vijukuu. Yeye ni Baba. Huna budi kuzaliwa mara ya pili! Yeye si eti Mtu mkubwa, mpole, aliyepungukiwa na akili.

171 Yeye ni Mungu mwenye kuhukumu. Biblia husema ya kwamba ndivyo alivyo. Hasira Yake ni kali sana. Usikanyage juu ya Hayo na kutarajia wema wa Mungu siku moja ukuchukue, katika dhambi zako, na kukupeleka Mbinguni. Kama angalifanya hivyo, basi angaliwasamehe hawa wote hapa, na amchukue Hawa. Utaamini Neno Lake, ama uta . . . utaangamia. Na unapoamini Neno Lake, Ishara itakuwa juu yako. A-ah.

172 Mauti yalikuwa tayari kuipiga Misri usiku huo, wakati wo wote. Ulikuwa wakati wa kuogofya sana; sherehe zao zote, sikukuu zao zote, na siku za kufunga.

173 Mungu aliwazuru. Mungu aliisha onyesha ishara Zake kuu na maajabu kati yao. Ni nini hiyo? Sasa tulieni kidogo. Mungu aliisha waonyesha neema Yake. Alikuwa amewapa nafasi.

174 Hawangaliweza kuikataa, na waseme, "Lo, hamna kitu hapo. Ni upuzi. Ni kitu fulani kule kwenya maporomoko ya maji, na kulikuweko na mlipuko wa matope me—mekundu yaliyorushwa juu, na hayo ndiyo yaliyosababisha ile bahari kuwa nyekundu." Kisha mawe ya mvua yakaja. Kisha wakaja vyura. Mungu alikuwa ameandaa mahali fulani, kisha akaweka Neno Lake katika kinywa cha nabii. Na aliyonena, yakatimia. Nao waliona hayo. Hawangaliyakana.

175 Kile alichoagiza Musa, ndicho alichopata Musa, kutoka kwa Mungu, kwa maana alinena tu Neno la Mungu. Alisema, "Nitakufanya wewe mungu." Musa alikuwa mungu kwao. Mnaona? Hawakujua lingine, kwa hivyo Yeye akasema, "Utakuwa mungu, na Haruni atakuwa nabii wako. Mnaona, utakuwa kama mungu, kwa maana nitakuchukua, sauti yako, nami nitaumba kwa kukutumia wewe. Nami nitanena, nao watu hawawezi kuikana, kwa maana ndiyo hiyo papo hapo. Utakalosema, litatendeka." Lo, jamani! Naam, basi. "Nitakuonyesha mambo hayo." Lo, Nayo Misri ikayaona. Waliyaona kabla tu ya wakati wa jioni, ama mnamo wakati wa jioni.

176 Aliwaonyesha wema Wake. Aliwaonyesha angeuondoa, kuponya.

177 Wachawi walijaribu kutenda jambo lile lile, waigaji. Utawaona kila wakati. Kulikuweko Yane na Yambre, wakisimama pale. Bali lilipofikia jambo lenyewe, hawakuwa nalo. Hiyo ni kweli. Walifuatilia, kitambo kidogo. Bali baada ya kitambo kidogo, upumbavu wao ukawa dhahiri kwa watu wote.

178 Je, Biblia haisemi jambo lile lile litatendeka katika siku za mwisho, "kama Yane na Yambre walivyopingana na Musa"? Lakini upumbavu wao ulifanywa dhahiri kwa watu wote, ndivyo itakavyokuwa tena. Mnaona? Naam, watu walioharibikiwa akili zao, wamekataliwa kuhusu kweli, Jambo lenyewe. Huenda wakawa na kusanyiko na mambo makuu na makuu, ya juu sana na mambo maridadi, bali ile saa itafika hatimaye.

179 Simameni imara na ile Ishara! Hivyo ndivyo Mungu anatutaka tufanye. Lishikeni Neno Lake. Msiliache. Kaeni nalo kabisa. Biblia inasema hivyo.

180 Mauti yalikuwa yakipiga. Mungu akawarehemu, akaonyesha uwezo na ishara.

181 Basi, hebu tukome kwa dakika moja ama mbili, kwenye ile saa kule. Hebuni tuwazieni tu akilini mwetu, nyuma, yale aliyoahidi yatatendeka katika siku za mwisho. Nashangaa iwapo haingalitupasa tujichunguze, pia, mnaona?

182 Yeye alikuwa ametenda mambo haya yote, hata hivyo hawakutaka kutubu, ama kuamini Ujumbe wa wakati huo. Wangali hawakutaka kufanya hivyo, hata ingawa ilikwisha onyeshwa mbele zao, na bila shaka ilikuwa imekwisha kutangazwa.

183 Nawe unapoona mambo kama hayo yakitendeka, ni dalili ya hukumu inayokuja. Hukumu itafuata mambo hayo. Imekuwa hivyo daima, na hii haitakuwa tofauti. Mnaona? Hukumu huifuata neema. Rehema inapokataliwa, hamna kilichosalia ila hukumu. Kwa hivyo itaifuata daima.

184 Sasa, mambo yenywewe. Kila tukio la kiroho ni ishara kutoka kwa Mungu. Iweni waangalifu. Tazameni hilo, mnaona. Tazameni, kila tukio la kiroho, kila kitu kinachotendeka, ni ishara. Hatuko hapa kwa bahati. Mambo haya hayatendeki kwa bahati. Ni ishara. Ni ishara, kuingia—ingieni mahali pa salama, upesi. Nuhu alikuwa ishara kwa kizazi chake; Elija alikuwa ishara kwa chake; Yohana alikuwa ishara kwa chake. Mnaona? Kila kitu, Ujumbe wa wakati huu, ni ishara. Uchunguze, tazama unachofanya. Unaona? Ni ishara. Kila kitu kina maana yake.

185 Na hapana wakati mwingine wo wote ambapo Ujumbe wa namna hii ungalizuka. Haungalikuja katika siku ya Luther, haungalikuja katika siku za Wesley, hata haungalikuja katika siku za Pentekoste. Haungalifanya hivyo. Mnaona? Hamna . . . hapajatukia jambo kama hilo, hata hivyo tuliahidiwa katika Biblia. Mnaona? Tuko katika wakati wa mwisho.

Hamna kingalitendeka, haingalitendeka hata wakati huu. Nayo inatendeka kama ishara. Nashangaa ishara ni nini?

186 Jamani, enyi watu wadogo, ndugu zangu, dada, ingieni chini ya Ishara hiyo, upesi. Mnaona? Msichukue, msichukue badilisho lo lote. Msifanye, msifanye, msifanye hivyo. Mnaona? Usiiwazie tu. Kaa mle hata utakapojua ya kwamba Ishara imekwisha pakwa, hata nia (yako yote) iliyokuwemo ndani ya Kristo iwe ndani yako, hata upuzi wote wa ulimwengu umeondoka, unaona, hata tamaa yote ya moyoni ni Yeye. Unaona? Hivyo, basi, unajua, ndiposa unajua jambo fulani linatendeka. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," si wanaojifanya waamini, bali waaminio. Unaona? Sasa, hatutaki kutwaa cho chote, kubahatisha juu yake; haikupasi kufanya hivyo.

187 Ujumbe wa wakati huu ni ishara kwa makanisa. Ni ishara kwa watu. Usi . . . je, mnafahamu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Natumaini, wanaosikiza kanda, ya kwamba wanafanya jambo lile lile, mnaona, na sehemu zingine ulimwenguni. Mnaona, Ishara ya wakati imewadia. Kuna ishara ambayo haina budi kupakwa, haingalikuja wakati mwingine wo wote.

188 Tazama matayarisho ya Mungu ya wakati huo. Sasa, tunajua ya kwamba Biblia ilisema, "Mambo hayo yote yalitendeka kwa jinsi ya mfano, mwaona, kwetu." Tazama, Mungu alipojiandaa kuihukumu Misri, kwanza alifanya matayarisho. Alifanyaje wakati wa kwanza? Yeye habadili utaratibu Wake.

189 Wakati wa kwanza, alipopata, alipofanya matayarisho Yake, alimtuma nabii akiwa na ujumbe. Jambo la kwanza alilowafanyia watu Wake lilikuwa kumtuma nabii mwenye ujumbe.

190 Jambo lililofuatia alilofanya, kumtambulisha huyu nabii, alituma Nguzo ya Moto kama utambulisho, kuutambulisha.

191 Na kitu cha tatu alichotuma kilikuwa ishara. Hiyo ni kweli kabisa. Ishara, hiyo ishara ilikuwa na maana gani? Dhamana!

192 Kwanza, nabii Wake mwenye ujumbe; Yeye alijitambulisha Mwenyewe miongoni mwa . . . kwa—kwa Nguzo ya Moto pamoja na nabii Wake, halafu akatuma ishara, kuingia chini ya hii damu, ya kwamba tayari alikuwa amekubali hili badilisho la mauti mahali pako. Kisha, Damu ilikuwa ishara ya kwamba alitazama, ya kwamba uliisha sikia ujumbe, ukaamini ile Nguzo ya Moto, na kwamba alikuwa amekubali lile badilisho alilokuwa amekuandalia, na ya kwamba ulikuwa chini ya ile damu ya ile kemia ya Uhai uliotoka kwa ajili yako. Jamani! Ni kamilifu vipi, ni jambo lililo kamilifu vipi, unaona, wewe uko chini ya damu.

193 Sasa uko chini ya Roho, chini ya Roho Mtakatifu. Unaona? Unaona? Unauamini Ujumbe wa siku hizi, unaona, unaamini ule u—u—u—u—uweza, ile Ngu—Ngu—Nguzo ya Moto. Unaamini hayo, unaona, na unafanya hivyo.

194 Sasa, angalia sasa, kuamini tu hakutoshi. Si—si... Kutembea karibu na mahali ilipo hakutoshi. Waona, hiyo ni kujiharibu zaidi. "Kwa maana yeye ajuaye kutenda mema naye hatendi, kwake ni dhambi." Unaona, hao waamini wa kuishia mpakani, Yesu alinena jambo lile lile.

195 Waebrania, sura ya 6, "Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kufanywa washiriki wa Roho Mtakatifu, na kulionja Neno zuri la Mungu, na zamani zijazo, wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamemsurubisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kuifadhehi ile Damu ya agano, ambayo kwayo walitakaswa..." Ile kemia pale hutakasa. Hiyo siyo Ishara. Damu siyo Ishara sasa. Uhai ndio Ishara.

196 Uhai huo haungalikuweko, kwa maana ulikuwa wa mnyama. Kemia ndiyo iliyokuwa ishara, ilikupasa kutia damu yenyewe mlangoni. Bali sasa ni Roho Mtakatifu. Tunafikia hilo, katika muda mdogo, kulithibitisha, unaona. Uhai ndio Ishara.

197 Uhai wako umeondoka, nawe umekufa, na uhai wako umekufa. Umefichwa katika Mungu, pamoja na Kristo, ukatiwa muhuri mle na Roho Mtakatifu. Ile nia iliyokuwemo katika Kristo imo ndani yako. Naye Kristo, na Biblia, na Neno, ni sawa. Hapo mwanzo kulikuweko Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Kisha nawe, na Neno, na Mungu, na Kristo, ni sawa. "Nanyi mkikaa ndani Yangu, na maneno Yangu yakae ndani yenu, ombeni mtakacho, kitatendeka." Mnaona?

198 Akaweka uwezo kinywani mwa Musa, kuenda kule na Neno Lake na kunena, kisha vyura wakaja; nena, vyura wakaondoka; nena, chawa wakaja; nena, uhai—chawa wakaondoka. Amina.

199 Hata hivyo ishara ilihitajika kwa Waisraeli wote. Israeli wote walihitaji hii ishara. "Basi nitakapoiona ishara, nitapita juu yenu." Loo, jamani, jamani! Ni dhamana jinsi gani!

200 Israeli wakipanda kutoka Misri, walikuwa mfano, wa kilicho asili ya mfano siku hii. Misri ilikuwa kanisa, na Israeli iliwakilisha Bibi-arusi. Basi kama vile Israeli walivyotoka Misri, vivyo hivyo Bibi-arusi anatoka kanisani. Mnaona? Kwa sababu, hapana budi kuwe na kitu fulani kule apate kutoka ndani yake, na hana budi kutoka kwake, kwa hivyo, kama ilikuwa mfano. Ka—kanisa liko kule Misri, ulimwenguni na dhambini, na halijali ka—ka—kamwe kuhusu Ishara yenu. Hata hawaiamini. Bali Israeli waliipenda, kwa maana ilikuwa wokovu kwao. Lo! Loo! Inapaswa kutufanya tuwe na furaha, inapaswa kuifanya mioyo yetu...Loo!

201 Ipakeni, kanisa! Msishindwe sasa. Sivyo? Msiache, msiache, msiache jua lichwe. Msi-, msi-, msi-, msipumzike, mchana na usiku. Msibahatishe. Haitawafaa kitu, enyi watoto. Haitawafaa kitu. Hamna budi kuwa na Ishara.

202 Mnasema, "Naamini. Naam, nami huenda. Mimi, naam, naamini Ujumbe. Mimi . . . " Hiyo ni sawa, lakini, hilo—hilo ni sawa.

203 Bali huna budi kuwa na Ishara! Je, mnasikia, Maskini ya Branham? Hamna budi kuonyesha wazi Ishara! Bila hiyo, kuamini kwako kwote ni bure. Unaona? Utaishi maisha mazuri; unasikiza Neno lisemavyo; unaenda kanisani, unajaribu kuishi ipasavyo; hiyo ni sawa, bali hilo silo. "Nitakapoiona Damu," hiyo ndiyo Ishara. Na Ishara hapa si . . .

204 Kwa maana, nini, i—ilimbidi kuona kemia yenyewe, kwa maana uhai uliisha ondoka, umetoka kwake, alikuwa mnyama.

205 Bali hapa ni Uhai Wake Binafsi uliokuwemo katika Damu. Nayo kemia ilikuwa tu ishara ama ishara ya utakaso, bali ule Uhai wenyewe ndio Ishara; kwa kuwa bila tohara, bila Ishara, wewe hata haumo katika lile agano. Kitu hicho chote hufanya kazi pamoja. Ukisema umetahiriwa kwa Neno, nalo pekee, basi utaamini Neno; kama unaamini Neno, basi Ishara haina budi kuja, kwa kuwa Yeye alisema, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Ndivyo hivyo. Lo, jamani!

206 Tazama basi yale maandalizi kwa ajili ya watu Wake wa nchi ya ahadi. Tazama yale aliyofanya. Kwanza, alikuwa na watu aliowaandalia nchi. Alikuwa amewaandalia nchi. Na sasa, aliwatumia matayarisho kwa ajili yake, kwa ajili ya watu wa nchi ya ahadi. Ilikuwa tu kwa ajili ya watu wale waliochaguliwa tangu awali kwa ajili ya hiyo nchi ya ahadi, . . . ? . . . Na vile alivyofanya hivyo, alimtuma nabii pamoja na ujumbe, akautambulisha kwa Nguzo ya Moto, na akatoa ishara kusudi wapate kujua yakini ya kwamba ilikuwa kweli. Hiyo ni kweli. Ilikuwa faraja yao.

207 Israeli, walipotoka Misri wakati huo walikuwa m—mfano. Hii ni asili ya mfano, wa Kanisa likitoka katika madhehebu. Naam, si wote wanaofanya dhehebu. Namaanisha Bibi-arusi. Waona? Watu wengine, kuna baadhi ya walio huru, walio wabaya kama wa madhehebu, wakati mwingine wabaya zaidi.

208 Nazungumza kuhusu Ishara iliyopakwa. Ishara hukubaliana na kila Neno. Waona? Haina budi kufanya hivyo, kwa maana ni Neno. Ni Uhai uliokuwemo katika Neno. "Maneno Yangu ni ya Kiroho; ni Uzima," kasema Yesu. Waona?

209 Musa alipoanza huduma yake katika Israeli, kwa ishara kuu, waona, Israeli walikusanyika upesi toka kila sehemu ya Misri kuenda Gosheni, wakirudi nyumbani kwao, kwa maana walijua kitu fulani kilikuwa karibu kutendeka. Lo, ni mfano jinsi gani!

Lo, wanakuja kutoka Mashariki na Magharibi,
Wanatoka nchi za mbali; (hiyo ni kweli, mmeusikia wimbo huo)
Kula karamu pamoja na Mfalme, kula kama wageni Wake,
Jinsi hawa wasafiri walivyobarikiwa!
Wakiutazama uso Wake uliotukuka
Unaometameta kwa upendo wa Kiungu;
Wabarikiwe washiriki wa neema Yake,
Watametameta kama johari katika taji Yake.

Lo, Yesu yuaja hivi karibuni,
Majaribio yetu yatakwisha wakati huo.
Lo, je, vipi kama Bwana wetu angalikuja sasa
Kwa ajili ya wale walio huru na dhambi?
Lo, je, ingalikuletea furaha,
Ama huzuni na kufa moyo kabisa?
Bwana wetu atakapokuja katika utukufu,
Tutamlaki kule juu hewani.

210 Kuonyesha wazi Ishara! "Nami nitamfufua katika siku za mwisho." Bila shaka! Tuko katika siku hizo.

211 Hao watu wakakusanyika Gosheni. Wao walikuwa tayari. Walijua jambo fulani lilikuwa karibu kutendeka. Wao walikuwa tu kama . . .

212 Wachukue bata, inapofikia wakati wa kukutanika, wote hukimbia pamoja. Wakati nyuki, na cho chote kile, wanapokuwa tayari, kuna akili ya asili inayowavuta.

Roho Mtakatifu huwavuta watu!

213 Jamani, wakati ulipowadia wa kushuka kwa hasira ya Mungu, kila . . . Hapa wanakuja bata wawili, dume na jike. Hapa wanakuja bata bukini wawili, dume na jike; hapa wanakuja farasi wawili, dume na jike; kitu fulani kinawavuta, wale waliochaguliwa tangu awali. Wengine wote wakaangamia. Jamani! [Ndugu Branham anapiga makofi]. Wengine wote wakaangamia! Bali wale waliousikia huo mvuto wa kuingia, wao walijua ile safina ilikuwa imeandaliwa. Ilikuwa ishara, ya kwamba mvua inakuja. Walijua mvua inakuja, haidhuru maonyesho yalikuwa nini na yale watu wengine waliyowazia. Wao walijua.

214 Kulikuweko na kitu fulani ndani yao, kilichosema, "Ingieni mle, upesi sana! Ingieni mle, kwa kuwa hapo ndipo mahali pekee tu pa usalama." Kwa maana, Mungu alimtayarisha nabii, akatuma ile safina kama ishara, kasema, "Ingieni mle," nayo mvua ilikuwa inakuja. Nao wakaingia mle, wawili wawili. Hao wanyama wote wakaingia, wawili wawili, katika safina, kwa maana waliingia chini yake. Haidhuru wengine . . .

215 Nao wote wasiokuwa ndani ya hiyo safina wakaangamia. Wote waliokuwa nje ya ile ishara, ya damu, wakaangamia,

kila mmoja wao. Na kila mmoja aliye nje ya Ishara, ya Roho Mtakatifu, ataaangamia.

216 Haidhuru ni mwema vipi, ni mshiriki wa kanisa jinsi gani! Kulikuweko na wengi sana katika siku ya Nuhu. Na kulikuweko na wengi sana katika siku za Musa; bali mtu aliyeshindwa kule kupaka damu, kama ishara, aliangamia. Wale ambao hawakuingia safinani, waliangamia. Wale wanaokosa kuingia katika Kristo, kwa maana Yeye ndiye Safina.

217 I Wakorintho 12, ilisema, "Kwa Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa Mwili mmoja." Ule wa siri, si kanisa; bali wa siri, si madhehebu, ule Mwili wa siri wa Yesu Kristo! "Kwa Roho mmoja," herufi kubwa R-o-h-o, Roho, "sisi sote tumezamishwa katika Mwili huu mmoja." Ndipo Ishara iko mlangoni, kwa maana wewe umo katika Kristo. Naye alikuwa Ndiye, Sadaka yako, Yeye aliyestahimili hukumu. Naye Mungu anapoitazama hiyo, Yeye hawezi kutenda neno. Wewe u salama salimini, kwa kuwa Mungu na Kristo ni Mtu yule yule, Roho alifanyika mwili akakaa kwetu. Na ndiye huyo hapo Mungu pamoja na Nafsi Yake, pamoja nanyi, watoto Wake Binafsi, katika Mwili ule. Naam, si kemia fulani, bali Roho! "Nitapita juu yenu."

218 Walikusanyika kutoka Misri nzima, wakakutanike mahali hapa pamoja, kusudi wapate kuwa chini ya hii ishara.

219 Nao wametoka kwa Wamethodisti, Wabatisti, Wapresbeteri, Waluteri, Wapentekoste, na kadhalika, kuingia chini ya Ishara. Jinsi hasa ilivyokuwa wakati huo!

220 Ni Nguzo ya Moto iliyowakilishwa kule. Mmoja akamwarifu mwingine, mwingine akamwarifu mwingine, mwingine akamwarifu mwingine, na, muda si muda, hapa hao wote wakaanza kuja. Wakaanza kuja, nao wakaitazama ile ishara ya Mungu. Wakasema, "Hukumu imewadia."

221 Kisha huyo nabii akasema, "Nimesikia kutoka kwa Mungu. Kutakuweko na Ishara. Nanyi mtatia damu mlangoni. Mchinjeni mwana-kondoo, mkatie hiyo damu milangoni, na hiyo ndiyo itakayokuwa ishara, kwa maana mauti yanakaribia kupiga."

222 Hebu niwaambieni leo, kama mtumishi Wake, isipokuwa ile Ishara iwe mlangoni, kuna mauti ya kiroho itakayopiga. Na makanisa yote yanaelekea kwenye lile—lile baraza, Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Yote yanaurudia Ukatoliki. Nao ni wale tu walio halisi, ambao wamezaliwa mara ya pili, ndio hawataingia!

223 Kumbukeni, si madhehebu yenu ya Kipentekoste, kwa maana tayari yamo mle ndani. Inaonyesha yamekufa! Yameangamia. Yalitoa sadaka. Yakarudi nyuma. Yalimtoa nje ya mlango, bali Yeye anatafuta Ishara. Kwa maana, jambo pekee walilotegemea lilikuwa kunena kwa lugha.

224 Usije ukategemea kabisa kunena kwokwote kwa lugha, wala cho chote kile. Bali hebu na Ishara Yenyewe iwe mle, Utu wa Yesu Kristo, Uhai Wake Binafsi ndani yako. Usitahiri tu *hili,* na *lile;* bali utahiri utu wote, mpaka wewe na Kristo muwe Mmoja. Kristo yumo ndani yako, na Uhai Wake unaishi kupitia kwako.

225 Sasa, sasa, kutoka Misri nzima! Na tazama sasa, tunapoona waliyotenda, tunapoona wakati ukiwadia, tumeagizwa kutenda jambo lile lile. Mlijua hayo? Tazama alivyosema nabii.

226 Na sasa tunasoma basi, mkitaka kusoma, katika Waebrania sura ya 10. Na mkitaka kusoma pamoja nami, nataka kusoma kifungu kimoja au viwili hapa sasa kabla hatujaendelea. Waebrania sura ya 10, na tuanzie kifungu cha 26 cha sura ya 10 ya Waebrania. La, mimi. . .Hebu tuone. Ndiyo. Naam, bwana! Waebrania, sura ya 10, na kifungu cha 26, mnaona.

> *Maana kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea. . .*

227 Hebu tuone, nimekipata hicho sawa? Naam. Sawa. Ndio.

> *. . .kama tukifanya dhambi kusudi baada. . . kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi;*
>
> *Bali kuna kuitazamia hukumu kwenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwaka kwa* wapinzani.
>
> Tazama hapa! *Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili ama watatu:*
>
> . . .ni *adhabu iliyo kubwa zaidi,* hata hivyo, kama ninyi, itakayomstahili *mtu yule aliyemkanyaga chini ya miguu, chini ya miguu Mwana wa Mungu, na. . . kuihesabu* agano la damu *aliyotakaswa kwako kuwa ni kitu ovyo, na kumfanyia jeuri Roho wa neema* aliyekuja kutoka kwa ile Damu?

228 Ewe mhudumu, mshiriki, mtu mwema, mtu mwaminifu, hata uwe nani, na wajua ya kwamba Mungu amekuondolea sigara. Enyi wanawake, mnajua ya kwamba amewaondolea suruali fupi, na—na nywele fupi, na kila kitu toka kwenu. Mnajua alifanya hivyo. Lakini basi ukigeuka na kuifanyia jeuri, kuihesabu ile Damu ya agano, kusema, "kitu kiovu," iliyokutakasa na kukuleta umbali huu!

229 Kama wale wapelelezi, kama walifika hapo mpakani, wakatazama kule ng'ambo, kisha wakasema, "Vema, najua iko, bali pingamizi ni nyingi sana. Tunajiona nafsi zetu kuwa kama mapanzi," waliangamia jangwani. Waamini wakwamia mpakani!

230 Usifikie tu umbali *huu*, ukasema, "Naamini Ujumbe." Tii Ujumbe! Ingia katika Kristo! Unasema, "Naamini kila neno

lililosemwa, Ndugu Branham." Hilo ni sawa, bali hiyo ni—hiyo ni uwezo tu wa kusoma.

231 Chukua Ujumbe, uingize moyoni mwako, ya kwamba huna budi kupata ile Ishara, Uhai ule ule uliokuwemo katika Kristo uwe ndani yako. "Nitakapoiona hiyo, nitapita juu yenu."

232 Tunapoziona zile ishara kubwa za wakati wa mwisho duniani leo, tunajua hiyo ni kweli. Sasa tazama, nimengojea huu kwa muda mrefu, mrefu sana, Ujumbe huu kwenu. Mnaona? Nanyi mmeziona zile ishara za wakati wa mwisho. Nami nimewahubiria Hilo, na kuwaonyesheni ninyi, kwa kila alichosema Kristo. Sivyo? [Kusanyiko linaitika, "Amina."—Mh.] Mtakubali hilo? ["Amina."] Tuko katika wakati wa mwisho. Sioni kilichosalia.

233 Mnasema, "Na ile alama ya mnyama, je?" Wale wanaomkataa Roho Mtakatifu, tayari wametiwa alama na yule mnyama. Hukumu itakuja baadaye. Mnaona?

234 Katika Israeli, baragamu ilipolia katika mwaka wa Sikukuu, kila mtu. . .Je, ulimwona Kristo, katika kusoma hilo? Alisoma tu nusu yake, kwa kuwa ni nusu yake tu iliyohusu wakati huo. Mnaona? "Alinituma kuwatangazia waliovunjika moyo, kutangaza uhuru, na kadhalika, mnaona," bali, Yeye, "na mwaka wa Bwana uliokubaliwa." Yaliyobaki, hakusoma—hakusoma hayo; akakiweka kile chuo chini, kwa maana hayo ni kwa ajili ya siku hizi. Mnaona? Alisoma tu sehemu yake, sehemu yake ilikuwa kwa ajili ya siku Zake.

235 Basi haya ndiyo atakayofanya leo. Haya ndiyo anayenena, kwa Roho Wake aliye na upako, kwa kanisa leo. Wakati umefika. Wakati ndio huu. Ipokeeni, enyi watu. ipokeeni.

236 Nini! Tunaziona zile nyakati kuu za mwisho, taa nyekundu zikimemetesha, kila mahali. Katika maumbile, tunaona maumbile yakimemetesha taa. "Wakati umewadia." Tunauona juu ya Kanisa, ukimemetesha taa. Limehukumiwa. "Wakati umewadia." Limo ulimwenguni. Tunauona mbi—mbinguni, baharini, juu ya mataifa, kila mahali; katika jua, mwezini, nyotani. Ishara!

237 Tunaziona ishara za wakati wa mwisho za Roho Mtakatifu zikiwarudia watu. Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, jinsi Roho Mtakatifu alivyotenda kupitia mwili wa binadamu pale, huyo alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Jinsi Mungu angejiingiza katika mwanadamu, Yeye Binafsi katika Bibi-arusi Wake katika siku hiyo, na kuonyesha ishara ile ile. Yesu alisema itakuwa vivyo hivyo katika siku za mwisho. Tunaiona. Tunaona Nguzo ile ile ya Moto. Hata sayansi imeipiga picha, na kadhalika. Tunaona ishara za wakati wa mwisho zimewadia. Tunajua ziko hapa.

238 Kisha, tunapoona haya, iwapo mnaniamini! [Ndugu Branham anagongagonga mimbara—Mh.] Kama hamniamini;

aminini zile ishara, aminini Neno, kwa kuwa zinanena habari ninayowaambia. Kama siwaambieni Ukweli, hazingalizungumza. Mungu hatazungumzia uongo kamwe. Mungu huzungumzia Ukweli. Na maneno haya yanashuhudia ya kwamba ninawaambieni Kweli. Ndiyo yanayoshuhudia Ujumbe ninaouhubiri. Si yule Malaika kule chini mtoni siku hiyo, ambaye alisema, "Ujumbe wako utakutangulia kule kuja kwa pili kwa Kristo," kazi zenyewe! Kama huwezi kuamini yule Malaika alisema Kweli; amini zile kazi, kwa kuwa Biblia ilisema mambo haya yatatendeka wakati wa mwisho. Ndizo zinazoshuhudia. Ndizo zinazonena kwa sauti kuu kuliko maneno yangu ama ya mtu ye yote yule. Ni Neno Lake. Zinashuhudia wakati huu.

239 Tunaona hizi ishara kuu na za kutisha juu ya watu, na ishara za wakati huu, duniani, na dhiki kati ya mataifa.

240 Tunaona Israel katika nchi yao. Ile bendera, ile Nyota yenye ncha sita ya Daudi, ikipepea, ndiyo bendera ya kale sana duniani, bendera ya kale sana ulimwenguni. Imekuwa taifa. Imekuwa na serikali. Ina raia wake. Iko kwenye Umoja wa Mataifa. Ina, ina, ina mambo haya yote. Iko kwenye Umoja wa Mataifa. Pia ina fedha zake yenyewe, kila kitu. Yesu alisema, "Kizazi hiki hakitapita, hata yote yatakapotimizwa." Pia, kumbukeni, usiku ule ule Israel ilipofanywa taifa, ni usiku uo huo yule Malaika wa Bwana aliponijia kule ng'ambo. Hiyo ni kweli. Sote tuko hapo.

241 Kila kitu kimeelekeza katika Kweli hasa. Sijawadanganya. Nimewaambieni yaliyo Kweli, naye Mungu ameshuhudia ya kwamba nimewaambieni yaliyo Kweli. Sasa, kumbukeni, mimi ni ndugu yenu. Mimi ni mwanadamu, mnaona. Mimi ni mwanadamu tu kama ninyi nyote, lakini mtu fulani hana budi kuuleta, mtu fulani hana budi kuusema. Hilo halikuwa chaguo langu; lilikuwa changuo Lake. Nami nimewaambia Kweli, naye amekwisha shuhudia papo hapo kwamba ni Kweli. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

242 Nasi tunapoona mambo haya duniani leo, lo, enyi watu, huu ndio ule wakati wa mwisho. Jivikeni hiyo ishara, upesi mwezavyo; au muingie katika Ishara, ingieni katika Ishara. Tunapoona ishara kuu ya mwisho, na wakati ukikaribia, ukituonya, "Wakati umewadia."

243 Jamani, chukueni hili kwa uchaji! Inatupasa kupendana sisi kwa sisi. Lo, jamani! Inatupasa kupendana sana! Msinene maovu ninyi kwa ninyi. Mtu akitenda kosa, mwombeeni upesi sana. Tuko pamoja katika hili, pamoja na Mungu. Sisi ni ndugu na dada. Jamani, ishini kitaua. Ishini, ishini kama binti za Mungu, ishini kama wana wa Mungu. Ishini mkiwa wazuri, wema, wanyenyekevu.

244 Hebu uovu wo wote usiingie mawazoni mwenu, katika fikira zenu. Uondoeni, tu. Ukipiga hodi mlangoni, uondoeni. Semeni tu, onyesheni tu Ishara yenu, endeleeni tu kutembea, "Niko chini ya Damu!"

245 Kumbukeni, kuna wengi sana waliokwenda kwa wale wanawake usiku huo, [Ndugu Branham anagongagonga mimbara—Mh.] wakasema, "Ewe, Gertie, Lillie, wengine wenu, tokeni twende, tunaenda kwenye karamu usiku wa leo."

246 "A-haa! mimi niko chini ya Damu. Nimo chini ya Ishara, kudumu humu. Upendo wangu ni kwa Muumba wangu. Mauti yamo mchini usiku wa leo."

247 Na mauti yamo nchini leo. Hukumu inangoja, ingali bado. Atomiki, hewa ya haidrojeni, na kila namna ya maangamizi, yanangojea mataifa.

248 Naye Mungu analiendesha Kanisa Lake, na kuonyesha yote. Tumekuwa tukimweka yule Mwana-kondoo mpaka sasa kwa muda mrefu, tukitazama, tukiona yale Yeye anayotenda, tukitazama tabia Yake na kila kitu, bali sasa Ishara haina budi kupakwa. Haina budi kupakwa. Hilo ndilo jambo pekee. "Mtu asipozaliwa kwa Roho na maji, hataingia kamwe." Na yawapasa kupendana. Waamini wanapaswa kujitenga na ulimwengu. Usiichukue sasa kwa urahisi.

249 Basi, ninyi watu mnaosikiza Hili, kwenye kanda, enyi wanawake, enyi waume sikizeni kwa dakika moja. Iwapo mlipata kuniamini mimi, aminini sasa.

250 Ni wakati wa kukomesha kuzozana mmoja kwa mwingine. Aminini Ujumbe wa Biblia! Aminini Yesu Kristo! Kisha pendaneni, stahianeni, na heshimianeni. Enyi wanaume waheshimuni wake zenu. Heshimuni nyumba zenu. Kusanya jamaa yako pamoja, kwa maana, kumbuka, huyu Mwana-Kondoo alikuwa kwa ajili ya jamaa, si mtu mmoja tu, ni jamaa nzima, pia, ilipaswa kuletwa. Kila kitu kilipaswa kuingizwa ndani. Inatupasa kupendana sisi kwa sisi. Nao waamini inawapasa kujitenga na ulimwengu.

251 Tazama, hawakuwa wamekusanyika kuzungumziana habari ya ujumbe. Walikutanika wapate kuitia ile damu, kuipaka ishara.

252 Hivyo ndivyo iwapasavyo kufanya. Mchungaji Neville, na kusanyiko hili, wadhamini, mashemasi, kwenu enyi ndugu, wakati umewadia kwetu kuweka kando upuzi wote wa ulimwengu, wakati umefika wa kuweka kando kila kitu. Tumeona ya kutosha sasa, hata tuna hakika, kabisa. Na Ishara haina budi kupakwa. Bila hiyo, utaangamia, huna budi kuangamia, hilo ndilo jambo pekee.

253 Jamani, msikusanyike, mkaseme, "Naamini." Ingia chini Yake, ingia ndani Yake! [Kukatizwa na mawimbi mafupi ya

redio kunasikika—Mh.] Unafanyaje hivyo? Kwa Roho mmoja tumebatizwa katika Mwili wa Yesu Kristo." Kila mtu aamini, kwa moyo wako wote. Mnaona? Yeye hakuhusika na mtu ye yote asiyekuwa chini Yake.

254 Ni nani huyo aliyekuwa akizungumza? [Mtu mmoja anasema, "Hiyo ilikuwa redio yenye mawimbi mafupi, Ndugu Branham."—Mh.] Mawimbi mafupi kutoka juu? ["Yakija kupitia kipasa sauti"] Yakipitia kwenye kipasa sauti. Nalimsikia mtu fulani. ["Ndugu Branham, naamini yalikuwa mawimbi mafupi yaliyoingilia kule nyuma."] Mawimbi mafupi, naam. Lo, wao—wao waliunganisha na redio. Nakisia wao . . . Lo, kwenye motokaa? Kunradhi. Najua mtu fulani alisema jambo fulani. Na nilifikiri mtu fulani alitaka kuniambia kitu fulani, nao hawakukipata, mwaona, na hiyo ndiyo sababu ni—nilisema niliyosema. Nilikuona ukitazama kila mahali. Nikasikia sauti. Nilifikiri mtu fulani aliinuka kusema jambo fulani, nami sikujua ilikuwa nini. Sasa, sasa, asanteni.

Lakini, aminini, ingieni chini Yake!

255 Israeli hawakukusanyika pamoja, wakasema, "Hebu sote twende zetu kule Gosheni leo. Tutaenda mpaka Gosheni. Panda juu ya ngamia wako, nasi tutachukua gari la ng'ombe. Kisha tutachukua akina Yona, hapa, na kadhalika, na—na akina Goldbergs, nasi tutapanda kwenda—kwenda Gosheni. Nanyi mwajuaje? Musa atazungumza leo." Haikuwa hivyo. La, bwana, ndugu! Ni, kuingia chini ya Damu! Naam, hasa,

Si kuzungumza habari Zake, kuingia ndani Yake!

256 Mmoja wao asema, "Unajua, Bwana Goldberg, bila shaka hiyo ni Kweli."

257 "Naam, ndugu, naamini ni Kweli. Najua hiyo ni Kweli."

"Bw. Levinski, unaonaje juu Yake?"

258 "Ni kweli kabisa. Naliona uweza wa Yehova aliye Mungu ukinena. Naliona hao chura wakitoka mle nchini. Najua hayo hayakutendeka hata aliponena, nami najua ya kwamba huyo ni Yehova aliye Mungu." Basi, hayo yote ni sawa.

"Je, umekwisha tahiriwa?

"Naam, bwana!"

"Wewe ni mwamini?"

"Naam, bwana!"

259 Ndiposa alipomsikia Mchungaji Musa akinena, siku hiyo, akasema, "Bali huna budi kuingia chini ya hiyo damu, kwa maana Mungu alisema, 'Ile damu ndiyo ishara.' Ni ishara! Haidhuru unaamini vipi, umetahiriwa vipi; hilo ni agano Mungu alimpa Ibrahimu, na kadhalika, hilo ni agano. Bali huna budi kuingia chini ya damu, hiyo ni ishara, kwa kuwa alisema, "Nitakapoiona damu, nitapita.' Israeli, ama ya yote yule!"

260 Uliye wa kidhehebu ama usiye wa kidhehebu, mmoja wenu, huna budi kuingia chini ya ile Damu. Mmethodisti, Mbatisti, Mpresbeteri, Mpotekoste, asiye wa kidhehebu, hata uwe nini, ni kwa ajili ya mtu binafsi. Huna budi kuja chini ya Damu. Naam, usizungumze tu habari Zake; ipokee! Nisikizeni! nisikizeni! Katika Jina la Bwana, nisikizeni! Mnaona? Lazima uingie chini ya Damu!

261 Yeye hakuhusika na mtu ye yote aliyekuwa nje ya hiyo damu. Mungu alifanya hayo dhahiri ya kwamba wote waliokuwa nje ya hiyo damu waliangamia.

262 Nitumie Maneno Yake? Wote walio nje ya Kristo wataangamia. Unaingiaje ndani ya Kristo? Wakorintho wa Kwanza 12, "Kwa Roho mmoja!"

263 Sio, "kwa kupeana mkono kumoja, kwa ushirika mmoja, kwa dhehebu moja." Hivyo ndivyo wanavyojaribu kuifanya. Huenda wakafanya hivyo.

264 "Bali kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja." "Kama malaika kutoka Mbinguni akihubiri cho chote kingine," Paulo alisema, "na alaaniwe." Huo ndio Ujumbe. Ingieni katika Kristo!

265 Tazama, mtu ye yote aliyekuwa nje ya ishara, Mungu hakuhusika. Na Mungu hahusikani na mtu ye yote, mkubwa kwa mdogo, anayependwa na watu wote au asiyependwa, tajiri kwa maskini, mfungwa ama aliye huru, mwanamume ama mwanamke; Yeye hahusikani na mtu ye yote asiye chini ya agano la ile Ishara. Hahusiki.

266 Unasema, "Lakini, Ee Bwana, nimefanya *hili*. Nalitoa pepo. Bwana, nalifanya *hivi*. Ni—nilihubiri Injili"

267 "Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Hata sikuwajua ninyi." Yeye hutambua tu Ishara.

268 Mnasikia hayo? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linaitikia, "Amina!"—Mh.] Basi, kwa hiyo ni juu yenu. Yeye . . .

269 Nilipokuwa nimeketi huko mwituni hivi majuzi, nao hao vijana walikuwa wanashangaa, kasema, "Siku mbili zimepita, bado wewe . . . " Hata sikumuua kindi. Kasema, "Kuna nini?" Mnaona, hivyo ndivyo ilivyokuwa. Mnaona?

270 Kasema, "Iweke juu yao, juu yao." Kasema, "Umezungumza—umenizungumzia habari zake." Mnaona? Sasa basi iko mikononi mwenu. Iko kwenu.

271 Yeye hatatambua cho chote ila hilo Agano, la Roho Mtakatifu. Nawe hauwezi kupokea hilo Agano isipokuwa umeokolewa, ukatakaswa, kisha ukabatizwa kuwa katika ule Mwili. Yeye hawezi.

272 Huenda ukawa na maigizo, huenda ukajisikia vizuri, ukaruka *juu chini,* na kunena kwa lugha, na kucheza katika

Roho. Hilo halihusiani nalo kamwe. Sikizeni, katika Jina la Bwana! Mungu hatambui hayo. Makafiri hufanya hivyo. Wachawi hufanya hivyo.

273 Unasema, "Mimi ni mwanachuoni. Mimi hufanya *hili, lile* au *lingine.*" Yeye hajali wewe ni mwanachuoni namna gani. Shetani ndivyo alivyo, pia, waona.

274 Yeye hutambua tu I—Ishara. Huo ndio Ujumbe wa wakati huu! Huo ndio Ujumbe wa siku hizi! Huo ndio Ujumbe wa wakati huu! Katika Jina la Yesu Kristo, upokeeni!

275 Si ba—. . .badilisho, kitu ambacho ibilisi anaweza kuweka juu yako; kama upendo haramu, kumfanya mwanamume kumpenda mwanamke mwingine mbali na mkewe, ama mke kumpenda mtu mwingine mbali na yeye, ama baadhi ya mambo haya hapa, jambo la aibu. Huo si upendo halisi. Huyo ni ibilisi. Hizo ndizo kazi zake. Ni kitu fulani amejaribu kukupa, badala yake; furaha, na kunywa pombe na kujisikia vizuri, kasema, "Nina moyo mzito; nitaenda zangu nikanywe vibaba viwili vya pombe, nipate kusahau." Hiyo ni mauti.

276 Mungu ndiye furaha yako. Mungu ndiye nguvu zako. Kujua Ujumbe. Kujua Kweli, huo ndio utoshelevu wetu sasa. Yeye ndiye utoshelevu wetu wote. Katika Yeye, mambo yote mnayohitaji yamo ndani yake. Huyo ndiye nguvu zetu. "Msaada wangu u katika Bwana." Enyi Wakristo, mtumainieni kwa ajili ya furaha yenu, mtumainieni kwa ajili ya nguvu zenu, mtumainieni kwa ajili ya furaha yenu. Yeye ndiye amani yangu. Yeye ndiye furaha yangu. Yeye ndiye upendo wangu. Yeye ndiye uzima wangu. Hilo ndilo Agano, Ishara mlangoni!

277 Yeye hawajibiki kwa mtu mmoja, mtu mmoja, hata uwe nani, Yeye hawajibiki kwa wale wasio chini Yake.

278 Na kumbukeni, jamaa yote ilipatikana, ikaletwa pamoja. Lo, jamani! Lo, kumbukeni!

279 Unasema, "Vema, baba yangu ni mhubiri. Ndugu yangu! Mchungaji wangu! Pia na. . . " Huenda hiyo ikawa kweli, pia, lakini na wewe je?

280 Kumbuka, walikuwa salama tu ile ishara ilipoonyeshwa! Kama mtu fulani alikuwa chini *hapa*, na mwanawe awe upande wa pili wa barabara, alikuwa hatarini. Angeangamia. Babaye angeokolewa. Ama iwapo mwanawe alikuwa *humu*, na babaye kule, babaye angeangamia. Ni ishara tu! "Nitakapoiona ishara, nitapita juu yenu." Hilo ndilo jambo pekee.

281 Unasema, "Vema, mwanangu ni mhubiri." Ninyi akina mama husema, "Mimi nina mvulana aliye mwema sana, ama msichana aliye mwema sana. Nawaambieni, hao ndio walio wema sana. Wao tayari wamejazwa na Roho Mtakatifu, na wana upendo sana! Wao ni watiifu. Sijapata kuona watu kama hao!" Nawe je, mama?

282 Unasema, "Mamangu ndiye mtu mzuri sana. Najua, akifa, ataenda Mbinguni, kwa maana yeye kweli ana Ishara, Ndugu Branham." Na wewe je, dada? Jamaa nzima haina budi kuwekwa chini yake.

283 Je, mmechoka! [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Nitamaliza tu kwa dakika chache, punde tu. Naweza kuukatiza na kuanza tena usiku wa leo. ["La."] Bali m—mkitaka kungoja muda kidogo zaidi, nitajaribu kuharakisha sasa. ["Amina."] Nitaweka hili ndani kabisa. Kwa maana, nafikiri, hivi sasa mnapokuwa na upako wake, ni vizuri zaidi kama mtaipata sasa hivi. ["Amina."]

284 Ni wakati tu Ishara inapoonyeshwa! Kisha, jamaa yote haina budi kuwa chini ya hiyo Ishara, Damu. Baba na mama, najua mnavyojisikia. Nina watoto, pia. Sina budi kuwaona wameokolewa. Ninajizungumzia mwenyewe leo. Mnaona? Nina ndugu zangu. Nina dada. Nina marafiki. Na—nataka kuwaona wameokolewa, pia. Bali, kumbukeni, bila kuonyeshwa kwa Ishara, wao wataangamia. Hamna ufufuo kwao. Hiyo ni kweli. Wamepotea. Ni wakati tu Ishara inapoonyeshwa!

285 Tazama, Yoshua, ningependa tungalikuwa na wakati wa kuisoma. Iandikeni, Yoshua sura ya pili; yule kahaba wa Kimataifa aliyeamini, Rahabu.

286 Jamani, ningependa ingalikuwa yapata saa tatu. Ningetaka—ningetaka kuchukua hilo na kuwaonyesheni jinsi hayo yalivyokuwa kule, mnaona. [Kusanyiko linasema, "Chukua wakati."—Mh.]

287 Huyu kahaba, Mtaifa, tazama, jamaa yake yote. Alikuwa mwamini. Jamaa yake yote ilipaswa kuingia chini ya hiyo kamba nyekundu, hiyo ishara. Walipaswa kuingia chini yake, la sivyo wangeangamia. Walikuwa wamekwisha kusikia kuhusu hasira ya Mungu. Waliisha sikia habari za kule kuonyeshwa kwa zile ishara na miujiza ya Mungu kati ya watu Wake, nao iliwapasa kuipokea. Ilimpasa kuipokea. Mungu, yule malaika wa Mungu wa kuangamiza, alikuwa yuaja. Walijua hivyo. Naye Yoshua alikuwa ndiye huyo malaika. Walikuwa tayari mstarini.

288 Vivyo hivyo kila taifa, ulimwenguni, liko mstarini mwa ghadhabu ya Mungu!

289 Maskini kahaba huyu aliisha sikia. Imani chanzo chake ni kusikia! Yeye alisema, "Nchi nzima inafadhaika kwa ajili yenu." Hiyo ni kweli.

290 Sasa, wale wapelelezi waliotumwa mle kufanya matayarisho, na kadhalika, yeye aliwaheshimu hao watu. Na, yeye, alitaka kuokolewa. Akasema, "Najua ya kwamba Mungu wenu ndiye Mungu, nami nimesikia mambo makuu ambayo amekwisha kutenda. Najua alivyomtendea Ogu, nami najua alivyoyatendea mataifa mbalimbali. Naona ya kwamba wale wanaomkubali wanaokolewa, na wale wasiomkubali

wanaangamizwa. Nami nataka kuishi," akasema. Jamani! Ndivyo hivyo. "Nataka kuishi." Kwa kuwa wao walimwona Yo-. . .

291 Yeriko ilikuwa imekwisha sikia yale Mungu alikuwa anafanya, bali hawakujali onyo.

292 Na hamna dhehebu nchini humu, kila mahali, ila lile ambalo limesikia yale Mungu anafanya. Hawataki kujali onyo.

293 Nguvu Zake kuu pamoja na ishara zimekwishaonyeshwa. Aliyofanya, Yeye alivuka Bahari ya Shamu, kana kwamba ilikuwa nchi kavu. Alisababisha, aliumba vitu, na kuwafanya vyura, na chawa, na viroboto kuingia hewani; akaviumba kwa Neno Lake, kupitia kwa nabii Wake. Hiyo haikuwa siri. Wanajua hayo.

294 Naye Rahabu akasema, "Nimekwisha kusikia hayo. Sitaki kuangamia pamoja na hawa wasioamini." La, bwana!" Alijua hukumu haina budi kufuata, kwa sababu wao walikuwa tayari kabisa. Alijua hayo. Kwa hivyo, wao wakamtengenezea njia ya kuiepukia.

295 Hapana shaka waliamini ya kwamba dhehebu lao kubwa la Yeriko lingeliweza kustahimili hasira ya Mungu, mnaona, dhehebu lao kubwa.

296 Hivyo ndivyo wengi wao wanavyodhania leo. "Lo, bila shaka Mungu hatafanya hivyo." Hivyo ndivyo Shetani alivyomwambia Hawa. "Lo, bila shaka Mungu hatafanya hivyo." Atafanya hivyo, kwa sababu alisema atafanya, unaona, na hilo ni Neno Lake. Naam, bwana.

297 "Mtu asipozaliwa!" "Na ishara hizi zitafuatana na hao waliozaliwa!" Mnaona? "Hivyo watu wote watajua ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu," na kadhalika, mnaona. Vema, walitaka kufanya hivyo. Lo!

298 Nini kilitendeka? Sasa walinyamazishwa. "Hamna ufufuo utakaotendeka hapa. Dhehebu letu halitadhamini kitu kama hicho. Hatutaki upuzi kama huo kati yetu. Namkataza kila mmoja wenu kuhudhuria huo mkutano." Ah! Yeriko, moja kwa moja katika msitari wa waliolaaniwa!

299 Lakini bila shaka kulikuweko vijana wa kanda waliojipenyeza mle mahali fulani, kwa ajili ya mzao aliyechaguliwa tangu awali. Wakaingia kisiri nyumbani mwake na kuanza kucheza kanda chache. Alifanya nyu—nyumba yake kuwa kanisa, wapate kuupokea ule ujumbe.

300 Wangali wanazo, mwajua. Ujumbe ukamfikia yule Mzao aliyechaguliwa tangu awali, kwa vyovyote. Hatujui jinsi ulivyoingia kule, bali ulifika kule, kusudi wenye haki wasiangamie pamoja na wasio haki. Mungu anashughulikia hilo, leo. Naam, kwa njia moja ama nyingine huingia mle kisiri.

Hatujui vipi. Ingawa hawataudhamini, bali mna Mzao fulani mle aliyechaguliwa tangu awali.

301 Mtu ye yote anayejua cho chote kuhusu Biblia, anajua ya kwamba huyo kahaba alikuwa amechaguliwa tangu awali. Bila shaka alichaguliwa! Yeye haku...Biblia ilisema, "Hakuangamia pamoja na hao wasioamini." Hiyo ni kweli. Bali yeye aliamini ujumbe wa wakati huo.

302 Naye Mungu akampa ishara, kwa wajumbe Wake. Kasema, "Chukua kamba nyekundu sana, ukaifungie kwenye..." Kasema, "Kumbuka, usipofunga hiyo kamba nyekundu hapo, au kuiacha hapo, ambayo kwayo tumeepukia, hatuhusiki kwa kiapo chetu." Nao wakasema, "Iwapo hamko chini yake, sisi nasi hatuhusiki." Jamani! [Ndugu Branham anapiga makofi mara tatu—Mh.] "Rahabu, kila mzao aliyechaguliwa tangu awali humu, nenda kule nje ukawatafute. Mlete babako, mamako! Kwa maana, tumetoka hivi punde tu, chini ya huo upatanisho, kule Misri, na kila kitu ambacho hatukuweka chini ya hiyo ishara kiliangamia. Rahabu, ninakupa dalili. Ni ishara." Nami ninasema, katika Jina la Bwana, kama kusema, iwapo mtaweka hiyo! Najua hijo habari, za huyo mjumbe. Namjua yule malaika wa ghadhabu, Yoshua. Ndiye mjumbe wa Mungu anayeangamiza. Ninamfahamu, naye anajua kutakuwa na ishara ya dalili. Nanyi ining'inizieni mle, nami nitawahakikishieni. Ninawaapieni." Kisha Mungu akaapa, pia, ya kwamba cho chote ambacho hakitakuwa chini yake kingeangamia, na wote waliokuwa chini yake watakuwa hai.

303 Na sasa, kiapo hicho hicho kiko leo, jambo lile lile, waona, "Sitawaacheni muangamie pamoja na wale wasiouamini Ujumbe huu." Na wao...

304 Yeye alisikia habari ya kazi iliyokwishafanywa, naye akaamini. Lakini, yapata, yeye alikuwa...Yeye pamoja na baba yake, na baadhi ya ndugu zake, au cho chote kile, ndio tu walioamini, katika mji mzima.

305 Waona walivyo wachache? Mmoja tu *hapa* na *pale,* jamaa ndogo itatoka katika mkoa mzima. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mk.] Vivyo hivyo sasa, tunanena mambo yalivyo. Tuna...Iwapo utaona vile jambo lenyewe lilivyo, huna budi kuona vile mfano ulivyo kuwa kwanza. Huna budi kuona vile kivuli kilivyo, ndipo utajua jinsi jambo lenyewe litakavyoonekana. Waona?

306 Nguvu Zake zilionyeshwa wazi. Hukumu ilikuwa inakuja. Hawana budi kuamini, kusudi wapate kuokolewa. Naam, bwana. Nao hawa wadogo...

307 Hawa watu wakaingia mle; hawa wajumbe, na—na kuwapata wale wazao waliochaguliwa tangu asili ambao waliamini. Alitumia nyumba yake kama kanisa, kuwapokea hawa wajumbe.

Wao hawangaliwaruhusu kuingia katika makanisa hayo. La, bwana. Mnaona? Kwa hivyo yeye . . .

308 Hawatawaruhusu ninyi, pia. Watawafukuzeni mkisema cho chote juu yake. Naam. Mnaona.

Walikusanya wote katika jiji lake, ambao waliamini, chini ya ile ishara.

309 Hilo ndilo hasa litupasalo kufanya leo. Ukitaka wapendwa wako fulani waokolewe, yafaa uwaingize ndani hivi sasa. Unaona?

310 Wakati laana ya Mungu ilipoliharibu hilo jiji kubwa, ile alama ya ishara iliisalimisha nyumba yake. Amina. Ni nini? Hiyo alama ilikuwa kwenye ishara yake . . . Ama, ile ishara ilikuwa juu ya nyumba yake, wakati jiji nzima lilipoporomoka kabisa. Ilikuwa nini? Ilikuwa nini? Yoshua, yule mjumbe wa Mungu! Mungu Mwenyewe alitambua ujumbe wa mjumbe Wake. Amina! [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili—Mh.] Iliuthibitisha! Iliuthibitisha. Wao waliutambua huo ujumbe. Yeye aliutambua ujumbe wa mjumbe Wake. Na wakati jiji lote lilipoporomoka kabisa, ile kamba nyekundu ya Rahabu ilikuwa mlangoni bado, na wengine wote walitoweka.

311 Ndiposa, mara baadaye, wakaondoka malaika wanaoangamiza wakaangamiza kila kitu kilichokuwa katika jiji lile, hamna hata chombo kimoja kilichosalia. Mtu mmoja alichukua chombo kidogo, naye akaangamia pamoja nacho, kutoka katika hilo dhehebu. Akachukua kitu hicho chote na kukiangamiza! "Alaaniwe mtu ambaye atajaribu kamwe kulijenga tena. Mzaliwa wake wa kwanza atakufa atakapoanza," na kadhalika. Mungu alikilaani hivyo, kitu hicho kikubwa kilichoukataa ule ujumbe wa ne- . . . ujumbe wa neema na rehema, walidhani walikuwa salama salimini.

312 Watu wengi hufikiri, siku hizi, "Maana mimi ni mshiriki wa kanisa, mimi ni salama salimini." Usiamini upuzi kama huo.

313 Huku, "Ile Damu itakuwa ishara kwenu." Roho sasa ndiyo Ishara kwenu, ule Uhai uliokuwemo katika Damu.

314 Vivyo hivyo, hebu na tuwazie ya kwamba, ishara ile ile waliyoitumia kule Misri, ishara ile ile ya uhai iliyokuwa Misri, iliyokuwa Misri, Mungu alitumia mfano ule ule kule. Yoshua, mfano mkamilifu wa Yesu, alikuwa mwaminifu kwa ile alama ya ishara ambayo wajumbe wake walikuwa wamehubiri. Yoshua, aliposema hivyo, alisema, "Usiiguse hiyo nyumba wala cho chote kilicho ndani yake. Imehifadhiwa kwa Bwana." Amina!

315 Mtaifa, kahaba, mzurura mitaani, bali alisikia na kuamini, naye akaweka ishara.

316 Haidhuru jinsi umedidimia dhambini, uliyotenda, hiyo si kitu. Weka ile Ishara. Ni kwa ajili yako. Ukisikia moyoni mwako

kuna kitu kinachokuvuta, ni kwa ajili yako. Paka Ishara. Naye Yosh-. . .

317 Neno *Yoshua* maana yake ni Yehova- Mwokozi." Vivyo hivyo *Yesu,* linamaanisha "Mwokozi." Naye, Yoshua, alipojua wajumbe wake. . .

318 Wajumbe wake walirudi, wakasema, "Nimezitii amri zako. Nasi tulimpata mwanamke kule, tulipozicheza kanda, wajua. Tulimpata mwanamke aliyeamini. Nasi tukamwambia, ya kwamba wote watakaokuja chini ya hiyo alama nyekundu kule nyuma, ile ishara, ingemaanisha. Sasa nimehubiri hayo. Je, utatimiza hilo, Yoshua?"

"Naliwatuma kufanya hivyo." Amina.

319 Na Mungu alipotimiza hilo, hiyo nyumba haikuporomoka. Ndiposa Yoshua aliposimama pale na kutoa ishara wakiangamize kitu hicho chote, wakaenda moja kwa moja, naye Rahabu pamoja na watu wake wote waliketi sawa, na mali zao zote, amina, amina, mali zao zote zilikuwa nyumbani, salama. Wao walisimama tu mle, na haikuwalazimu kuchungulia dirishani. Wangalisoma Maandiko huku vita vikiendelea.

320 Mwanamke akarudi akaposwa, akaposwa na Jemedari jeshini, na akatunzwa, akaja Bethlehemu, na akagawiwa sehemu yake kati yao. Naye akamzaa. . .akamzaa mwana wa kiume mashuhuri, naye huyo mwana mashuhuri akamzaa mwana mwingine mashuhuri wa kiume, naye huyo mwana akamzaa mwana mwingine mashuhuri wa kiume, mpaka yule Mwana mkuu na mashuhuri alipokuja. Tangu kule nyuma, na kuendelea hata Obedi, na kuendelea kupitia kwa Yese, hata kufikia Daudi. Hiyo ni kweli, kahaba Rahabu, kwa kuwa alimwamini yule mjumbe. Akaweka ile ishara, nayo nyumba yake ikaokolewa, ama angaliangamia kule chini alikokuwa.

321 Sikizeni kwa makini sasa. Lo, nasema, mnaitambua? Wote waliokuwa chini yake waliokolewa kule Misri. Wote waliokuwa chini yake waliokolewa kule Yeriko. Wote walio chini yake wataokolewa leo. Yule mwenye damu, yule mwana-kondoo mwenye damu, ni mfano wa Yesu Kristo.

322 Katika Waebrania 13:10 na 20. Sina wakati wa kuisoma. Iandikeni. Nilitaka kuisoma. Inaitwa "agano la milele." Damu ya Yesu Kristo inaitwa "agano la milele." Naam, bwana! "Agano la milele."

323 Mbona haikuitwa "Agano lisilo na mwisho"? Kwa kuwa halingalikuwa lisilo na Mwisho. Tunapokombolewa, yote imekwisha wakati huo. Ni la *milele,* ambayo maana yake ni, "muda fulani wa wakati," hata wakati utakapokwisha. Hakutakuweko lingine kamwe. Wakati utakapokwisha hatutahitaji agano. Lakini mpaka wakati utakapokwisha, tunahitaji agano.

324 Basi, kumbukeni, Waebrania 13:10-20, “agano la milele.” Ahadi ya Mungu yenye masharti ya Damu inatufanya huru toka dhambini. Amina! Hamna dhambi ndani Yake; dhambi, ubinafsi, mwili.

325 Mwabuduni na muonyeshe uweza Wake ulioahidiwa! Watu, waliofungwa kwa Damu, waliofungwa kwa Ishara, wana Roho wa Yesu Kristo ndani hapa, kwamba, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya,” wakionyesha lile agano. Waona?

326 Agano Jipya! *Agano* maana yake ni “mapatano.” Hilo ni sawa, ama sivyo, Daktari Vayle? *Agano* maana yake ni “mapatano.” *Agano Jipya* maana yake ni “mapatano mapya.” Agano la Kale lilikuwa yale ya zamani, chini ya mwana-kondoo, ambapo ule uhai haungalimrudia mwamini. Agano Jipya lilikuwa Mwana-Kondoo wa Mungu, na uhai Wake huturudia sisi. Damu ni Uhai! Mnaona? Damu ni Uhai katika Agano Jipya, waona, Uhai hutoka katika Damu ya Mwana-kondoo, ambayo maana yake ni Agano Jipya, patano jipya.

327 Ya kwamba, Mungu, “Baada ya siku hizo, nitaandika amri Zangu juu ya kibao cha nyama ya mioyo yao.” Waona? Waona? “Si juu ya vibao vya mawe, na vya damu ya mwana-kondoo, ambapo mlipaswa kusema, ‘Naam, ni—nina damu upande *huu*, sasa inasema tufanyeje?’ Bali juu ya vibao vya moyo wako, waona, agano la Roho nitakalofanya pamoja na watu.”

328 Nalo huonyesha nguvu Zake. Yohana 14:12, inasema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.”

329 *Agano Jipya* ni “mapatano mapya,” Uhai mpya, inaonyesha ya kwamba Yesu ametimiza kila masharti kwa ajili yetu ambayo Mungu alihitaji, kutufanya tena, kweli, wana na binti za Mungu, chini ya ile Damu, ambapo hakuna tena hukumu ya adhabu.

330 Warumi 8:1, “Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika,” si wale *wanaoiamini,* “hao walio katika Kristo Yesu, hao ambao huenenda si kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho. Na Neno Langu ni Roho, tena ni Uzima.” Waona? Jamani, ningalitoa somo humo, na kukaa nalo kwa masaa kadha. Bali tutaharakisha, mnaona.

331 Hakuna tena hukumu ya adhabu, huru na dhambi, huru na shughuli za dunia, hakuna hukumu ya adhabu. Kwa nini? “Kwao hao ambao, kwa Roho mmoja, wamebatizwa kuwa Mwili mmoja.” Humo ile Damu ya Mwana-Kondoo imepakwa. Mungu wa Mbinguni amekukubali, na . . . Uhai Wake umo ndani yako, nanyi ni wana na binti za Mungu.

332 Tabia yako ni tabia ya Mungu. Ni nini, kusukumwa kudogo? La, bwana. Mungu ni Mungu wa hukumu. Ni Mungu wa kusahihisha. Hapana budi iwe sahihi. Hakuna kingine kitakachofaa. Hiyo ndiyo tabia yako, kwa sababu wewe una tabia ya Baba yako. Unaona?

333 Nini? Ule Uhai, tazama wakati (huo) uhai unapochokuliwa, badala ya damu. Waona? Uhai wenyewe ndio unachukuliwa. Unaona? Ule uhai, unatwaliwa, badala ya damu. Unaona? Ile damu ilipakwa, nao huo uhai haungalimrudia mwamini wakati huo, maana ni uhai wa mnyama. Sio uhai . . .

334 Bali, tazama, badala ya mwanadamu, ilikuwa Kiumbe cha hali ya juu sana, sana, sana. Mnaona? Na hiyo inamfanya mwanadamu sasa, si mwanadamu tu, bali mwana na binti wa Mungu, aliye na Uhai wa hali ya juu sana, sana, sana, sana, ambao uliokuwa ndani Yake, na kukurudia wewe; na unakubadilisha kutoka mwenye dhambi, na mambo ya ulimwengu, mshiriki wa kanisa, na mfuasi wa kidhehebu, ukawa Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, akajazwa Roho; na uhai wa Mungu ukimiminika tu kutoka kwako, kama spaki kutoka kwenye fuawe, unapoenenda, huku umejaa nguvu, upendo, upole, na Roho Mtakatifu akitenda kazi, akinena. Lo, jamani! Ndivyo hivyo. Na ukiwa na (nini?) Ukisikia Ujumbe, ukitazama ile Nguzo ya Moto, na dhamana yenye baraka, "Nimepita mautini kuingia Uzimani." Tazama, basi, hamna hukumu ya adhabu kamwe.

335 "Kama mioyo yetu haituhukumi, ndipo tumepata tuliyoomba, mwaona, tunajua." Bali kama mna dhambi mioyoni mwetu, basi inatuhukumu, basi—basi afadhali hata tusianze. Mnaona? Huna budi kuwa huru kutoka dhambini. Na njia pekee unayoweza kuwa huru na dhambi ni kuingia ndani Yake. Hicho ndicho kifuniko pekee cha dhambi, ni Kristo.

336 Kumbukeni, Damu ya agano, Damu ya agano haitambuliwi bila Ishara. Hauwezi. Hautaweza. Unasema, "Vema, ni—nimetakaswa kutoka kwa mambo." Hiyo siyo Ishara. Ni Roho, ndiyo Ishara, Roho wa Kristo juu yako. Iamini!

337 Sasa, tazama, Neno linatuhakikishia ahadi. Haya yote ni mafungu nimeyaandika hapa chini. Nitaendelea tu kuhubiri siku nzima, yaonekana, mnaona, juu yake. Mnaona? Neno linatuhakikishia ahadi, kwa maana Ndilo ahadi. Neno ndilo Ahadi, nalo Neno ni Mungu, na Neno ni—ni letu. Nasi tunafanyika Neno, nalo Neno linakuwa sisi. "Nanyi mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu," basi, mnaona, inakuwa jamaa moja kubwa mno. Mnaona. Linatuakikishia, kwa sababu gani? Vema, ni sehemu yetu. Mnaona? Mnaona? Mnaona, linakuwa sehemu yetu. Ni somo tamu jinsi gani! Vema. Linatuhakikishia, ahadi.

338 Ile Ishara ni dalili ya kwamba ununuzi umekamilika na umekubalika. Naam, huwezi kupata ishara ya gari la moshi mpaka umelipa nauli; na njia pekee utakayolipia hiyo nauli ni kulipa tu. Hiyo ni kweli. Vipi? Iamini, Ikubali. Utii mkamilifu wa Neno lote la Mungu utakustahilisha ile Ishara. Utii mkamilifu! Si sehemu yake kadiri liwezavyo dhehebu lako, bali lote.

Utii mkamilifu wa Neno, ambalo ni Kristo, unakuingiza katika Kristo.

339 Sasa vipi kama mwili wote ulikuwa ndani, bali miguu yako inaning'inia nje? Je! vipi kama mwili wote ungalikuwa ndani, huku mikono ikining'inia nje? Karibu sisi sote tuwe ndani, bali mioyo inaning'inia nje? Unaona? unaona? Moyo uwe ungali ulimwenguni bado? Mnaona? Bali sisi hatufanyi hivyo.

340 Utii mkamilifu kabisa unakufanya wewe na Neno kitu Kimoja. Unaliamini, lote kabisa. Nalo lote liko ndani yako, na ulione likifanya kazi kupitia kwako.

341 Huambatani na kundi linalofanya yasiyofaa. Unaona? Wewe ni Mristo. Hata mtu asema nini, hawatakugusa kamwe. Wewe umo katika Kristo. Wewe ni salama salimini.

342 Mauti yanapopiga hodi mlangoni, hayawezi kukushikilia, waona, hata kidogo. Kwa nini? Ni kukanyaga toka *hapa* hadi Pale.

343 Uzee haumaanishi kitu. Wewe umepita kutoka uzeeni. Umo katika Umilele, kwa maana umo ndani Yake. Yeye ni wa Milele. Haumaanishi kitu, iwapo wewe ni kijana, mzee, umri wa kati, au cho chote ulicho. Mwenye sura nzuri, baya, mfupi, mnene, cho chote kile, si hoja. Si kitu.

344 Hutangatangi huku na huko, na mambo haya mengine yote. Wewe, wewe umepita hayo. Umekufa. Uhai wako umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Umetiwa muhuri mle ndani na Roho Mtakatifu, ukitembea katika Kristo. Kitu unachoona tu ni Kristo. Hayo tu. Hayo pekee, unatembea. Lakini, lo, jamani! Sio ajabu tulizoea kuimba huo wimbo mdogo!

> Ijaze njia yangu kila siku na upendo,
> Ninapotembea na yule Hua wa mbinguni;
> Hebu niende muda wote, huku nikiimba na kutabasamu,
> Ijaze . . .

345 Hebu na niwe ndugu. Hebu nikaishi kama kielelezo cha jinsi Kristo alisema inampasa mtu kuwa. Hebu niwe ndugu kwa ndugu, ndugu kwa dada. Hebu niwe mu—muhudumu kwa wahudumu. Hebu niwe mfano wa mifano. Hebu nikauonyeshe ulimwengu ya kwamba hili Neno ndilo Kristo. Na vile ninavyoweza kufanya hivyo ni kuingia ndani Yake. Kwa maana, siwezi kufanya hivyo mimi binafsi, hauwezi kufanya hivyo. Bali hebu wewe pamoja na Neno muwe Mmoja, ndiposa litaishi Lenyewe. Wewe ni waraka unaotembea wa Yesu, anapochukua mamlaka yote, kukuongoza, kufanya kila Neno.

346 Kama akija *huku*, "Nataka kufanya Hivi," nawe unasema, "La, la, siamini Hilo", unaona, wewe hauko katika Neno bado. Unaona?

347 Mkamilifu, sasa tazama, kabisa, sasa, utii mkamilifu wa Neno lote la Mungu unatustahilisha Ishara. Kisha tunapolipa, tunapoomba, inatupasa kuwa na ile Ishara tupate kuitoa pamoja na maombi yetu.

348 Kama ukisema, "Naomba, Bwana, bali kweli sina..." Vema, huna. Hata afadhali ungelikoma, unaona, ku-...Endelea, kwanza, pata ile Ishara, waona, maana hiyo Ishara ndiyo Yeye atakayotambua. Unaona? Naam, bwana!

349 Tunapoomba, basi inatupasa kuonyesha Ishara, "Bwana, nimekutii Wewe, kabisa. Nimezitubu dhambi zangu. Najisikia ya kwamba Wewe umenisamehe. Nimebatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Roho Mtakatifu yuko juu yangu. Sasa ninahitaji kitu fulani kwa utukufu Wako. Bwana, nakiomba. Ni changu sasa." Kisha mna kitu fulani kinachotia nanga *huku* nyuma, "Whiu-whiu," ni chako. Hilo latosha. Ndipo imekwisha. Imekwisha. Imemalizika. "Naomba *hiki*. Nakiomba. Sharti nikipate. Mwaona? Mwaona? Na—nakitaka kwa utukufu Wako." Mnaona? Vema hivyo tu, ndipo anakupa tu. Basi unajua ni chako. Hivyo ndivyo ilivyo, watoto wetu, na kadhalika, tunapaka ile Damu, tunaamini. Hayo tu. Sawa.

350 Yeye anafanya nini basi? Ukisha, unapoweza kutoa Ishara pamoja na maombi yako, inaonyesha ya kwamba umetii kikamilifu Neno lote la Mungu. Unapokuwa na Ishara, inaonyesha ya kwamba umekwisha kutii kila Neno. Halafu, wewe na Neno ni mmoja, unaomba tu kitu kile ulicho wewe. Unaona? Unaona? Basi, kwa nini, unajua.

351 Kama nikiuambia *huu*, "Mkono, hebu unitii, chukua ile leso!" Unafanya hivyo. Unaona, mkono ulinitii. Kwa nini? Ni sehemu yangu. Unaona?

352 Basi wewe na Neno mnapokuwa Mmoja, kila ahadi, Mungu atukuzwe, kila ahadi ni yako. Inakutii. Ndiposa inakubidi kuangalia sana unachotaka kufanya. Hautautia mkono wako motoni, kusudi useme, "Oneni nikifanya hivyo." Loo, la, la, Unaona? Bali iwapo mna kitu mle motoni, ninachotaka kukitoa, utanitii. Unaona? Unaona? Hiyo ni kweli. Waona, inakupasa kuwa mwangalifu sana kwa yale unayofanya.

353 Hiyo ndiyo sababu Roho Mtakatifu hutolewa kwa kiasi, na kadhalika, mnajua ninayomaanisha, kwa maana wengine... Hautaki ku-...Mtumishi halisi wa Mungu hajidai na Roho, mwaona. Hayo tu. Huku ni kujigamba.

354 Tunapoomba, tunatoa ile Ishara. Inaonyesha ya kwamba tumetii kikamilifu.

355 Paulo anatuambia, ya kwamba, "Damu hunena." Kwamba, mtu ye yote anajua ya kwamba damu ni, kwa kweli, yenyewe, haiwezi kunena. Ni kemia. Sivyo? Wangapi wanajua hayo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Lakini ni wangapi wanaojua ya kwamba damu hunena? ["Amina."] Ukitaka

kuandika hilo, Mwanzo 4:10. Mungu alisema, "Na Ndugu yako je?" Kasema, "Damu yake inalia kutoka ardhini, dhidi yako." Amina! Sivyo? Damu yake inanena. Haleluya! [Ndugu Branham anapiga makofi mara tatu]. Mungu alisema, "Na yeye je?"

Akasema, "Mimi ni Mlinzi wa ndugu yangu?"

356 Akasema, "Damu yake inalia. Damu yake inalia." [Ndugu Branham anagongagonga mimbara mara sita—Mh.] Ni ishara. Ni ishara, ya kwamba amekwisha uawa. Damu yake ilikuwa ikilia dhidi yake.

357 Basi, ukipata hiyo katika Mwanzo 4:10, halafu katika Waebrania 12:24, anza kusoma. Katika Waebrania 10, 12:24. Kasema, "Damu ya Yesu inanena mema kuliko ile ya Habili."

358 Waona, Habili, yeye alikuwa mtu mwenye haki. Akafa. Akafa, bila hatia, kwa maana alikuwa katika Njia. Alikuwa katika Njia, akisimamia ufunuo halisi aliokuwa nao. Alinena. Ililia! Ile damu yenye haki ya Habili ililia dhidi ya Kaini.

359 Lakini Damu ya Yesu Kristo, haikulia tu, bali ilitukomboa. Amina! "Inanena mambo mema zaidi." Huwafanya ninyi wana na binti. Huwaficha toka kwa hasira ya Mungu. Unaona? Damu ya Habili haingalimficha Kaini, waona, bali Damu ya Yesu inaweza. Amina!

360 Kwa hivyo, Kaini, wa kale utoke leo, kama umekuwa mtesi wa Neno, na kusema, "Siku za miujiza zimekwisha. Kitu hiki chote ni upuzi kabisa, na kadhalika."

361 Inalia, waona. Damu ya Yesu inalia, bali ina msamaha iwapo utaikubali tu. Ningependa tungalikaa muda kidogo kwa hilo, "Ile Damu hunena mambo mema zaidi."

362 Aminini, kwa usalama. Kisha muipake, mnaona. Aminini kwa ajili yake. Hii ndiyo sababu ya kuiamini. Unaona, unataka usalama wako. Amini upate kuwa salama, ndiposa uipake Ishara kwa ajili ya jamaa yote. Unaona? Unasema, "Nawezaje kufanya hivyo?" Idai! Kama ilifanya kazi ndani yako, basi wewe na Neno mnakuwa mmoja. Amina! Amina! Unaona? Waona, inafanya kazi kwenu wawili. Wewe na Neno ni mmoja, kisha uipake kwa watoto wenu, uipake kwa wapenzi wako.

363 Kama vile Rahabu alivyofanya, aliweka ile ishara kwa baba yake, akaiweka kwa mamaye, akaiweka kwa ndugu zake na dada zake, naye akawaingiza wote ndani.

364 Itumie, useme, "Bwana, nitamleta mwanangu. Nitamleta binti yangu. Namdai! 'Shetani, mwachilie!' Naja kumchukua. Natumia Ishara yangu, Roho Mtakatifu. Ee, Roho Mtakatifu, uishiye ndani yangu, mshike binti yangu pale. Naenda kwake sasa, nikiwa na upako Wako juu yangu." Yeye atafanya hivyo. Amina.

365 Hivyo ndivyo walivyofanya kule Misri. Ndivyo walivyofanya Yeriko.

366 Ukitaka kusoma jingine, Matendo 16:31. Paulo alimwambia yule akida, "Amini! Mimi ndiye mjumbe wa wakati huu. Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe pamoja na nyumba yako mtaokoka." Sivyo? Amini kwa ajili ya nyumba yako, walete wote chini yake. "Sasa umemwona Mungu wa Mbinguni akifanya miujiza. Ni kabla ya hukumu. Mnaamini?"

"Naam! Nifanyeje?"

367 Akasema, "Inuka ukabatizwe." Paulo akamchukua akambatiza, kasema, "Basi mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako."

368 Kuamini nini? Mwamini Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya nyumba yako, ipake Ishara nyumbani mwako.

369 Ndiposa unafanyaje unapoipaka nyumbani mwako? Toa takataka yote nje. Ondoa rinda fupi zote, kaptura, na karata, na sigara, na televisheni, na kadhalika, ukaviondoe nyumbani, uendapo kutumia ile Ishara; hutakaa kimya kwake. Naam, bwana. Toa yote nje. Dansi zote, na karamu, rumba, na magazeti machafu ya kale, na mambo yaliyo ya ulimwengu, yapige teke nje ya mlango, ukaseme, "Tunafagia mahali hapa pote."

370 Kama Yakobo alivyofanya, alisema, akamwambia mkewe na wengine wote, kasema, "Fueni nguo zenu na kadhalika. Waondoeni hao miungu." Amina. Yo-. . .

371 Unajua Yoshua alivyosema kabla hawajavuka? Alisema, "Fueni nguo zenu; msiwakaribie wake zenu, na kadhalika, mkajitayarishe, kwa maana katika muda wa siku tatu tutauvuka Yordani." Amina. Alikuwa akijitayarisha, walikuwa wakipaka ile ishara. Amina. Ndivyo hivyo.

372 Jitayarishe. Ipake. Iamini. Jitakase. Hebu na watoto wako, hebu na jamaa yako, hebu na watu uwapendao, waione ndani yako. Hiyo ni kweli. Itatenda kazi. Naam, bwana!

373 Kisha ipake Ishara kwa maombi, kwa—kwa—kwa uangalifu, na kwa kuamini. Ipake kwa upendo mwingi, na kadhalika, hata utakapojua ya kwamba itatenda, itatendeka. Hivyo tu. Ipake kwa ujasiri, ukiamini itasaidia. Unapozungumza na huyo mtoto, unapozungumza na mumeo, unapozungumza na mkeo, ukizungumza na huyu mpendwa, amini ya kwamba itasaidia. Simama pale tu, ukaseme, "Bwana, nimewadai hao. Hao ni wangu. Nitawaleta Kwako, Bwana."

374 Ipake kisha ufanye hali kama hiyo ikuzunguke wewe, hivi kwamba wataingia tu mle ndani yake. Mwaona? Lo, wewe, wewe, kama una Ishara, unafanya roho kukuzunguka, nguvu fulani, hata unapotembea, watu wanajua ya kwamba wewe ni Mkristo. Wanataka sana uwaambie jambo fulani. Wanaamini neno lako. Yale usemayo, wanayashikilia. Unaona? Hivyo tu.

375 Paka ishara, kisha utembee nayo. Wadai walio wa nyumba yako. Huna budi kufanya hivyo sasa. Huu ni wakati wa jioni.

Sasa, mmekuwa mkinisikiza kwa muda mrefu, sasa huu ni wakati wa jioni. Ni wakati wa kuipaka sasa. Ile hasira itashuka, mojawapo ya siku hizi, huenda ikawa imechelewa sana wakati huo. Unaona? Ipake Ishara, kwa ujasiri.

376 Ukitaka kusoma hayo, soma jambo fulani hapa, Maandiko yangu niliyoyaandika kwa hilo, ni kusoma Waefeso 2:12, ukitaka kuandika hayo. Tazama, katika Waefeso 2:12, utakapoisoma, inasema haya. "Ya kwamba hatuzitumikii kazi zisizo na uhai, bali tunamtumikia Mungu aliye hai, kwa kazi zilizo hai." Amina! [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili—Mh.] Jamani! Kwa kazi zilizo hai, ishara zilizo hai. Mnaamini katika ishara zilizo hai? [Kusanyiko linasema, "Amina."] Pia, andikeni, Waebrania 9:11-14, mkitaka kuandika hilo. Ishara zilizo hai, kazi zilizo hai, tumieni hizo!

377 Si kanuni za imani zisizo hai, "Nitampeleka mvulana wangu kanisani, nione iwapo atajiunga na kanisa."

378 Mvulana fulani Mkristo aliye mzuri hapa, rafiki yangu sana, rafiki msiri wangu, mtu halisi, ali—alikuja humu, akabatizwa. Mamake akasema, "Ningependa ungalienda kwa kanisa kubwa zaidi iwapo ulitaka ku—kubatizwa." Unaona? Unaona, hakutaka tu kanuni za kale za imani na kadhalika. Mnaona?

379 Sisi hatuzitumikii kanuni za imani zisizo hai na miungu isiyo hai. Tunamtumikia Mungu aliye hai ambaye Damu Yake ilimwagika kule nyuma, nayo ile ishara imepakwa kwetu, kusudi tupate kuishi pia. Amina. Naam, bwana!

380 Msizitumikie kanuni za imani zisizo hai. Wao hata hukana vitu kama Ishara. Wao husema, "Siku za miujiza zimepita. Hamna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu." Mbona mkajiunge na kitu kama hicho? Mnaona? Msifanye hivyo.

381 Ipakani Ishara, kisha, "mkamtumikie Mungu aliye hai," kwa ajili ya kazi zilizo hai, ishara zilizo hai; ishara zinazowaponya wagonjwa, zinazowafufua wafu, zinazotabiri mambo, kunena kwa lugha, zikafasiriwa, kila wakati ni kweli kabisa, zinazotabiri na kusema *hili* na jambo *fulani* litatendeka, zinaonyesha ishara katika Mbingu juu, na duniani, ishara na maajabu, amina, zikinena hasa yale Biblia ilisema yatatendeka. "Mtumikieni Mungu aliye Hai," pakeni Ishara!

382 Usihudhurie hayo makanisa na kujiunga na kazi hizo zisizo hai na vitu kama hivyo, kwa maana hata hawaamini vitu kama ishara. Bali sisi ambao tunaamini, amina, tunajua Hayo. Wao husema, "Hamna kitu kama ishara. Hilo, lo, lo, huo ni upuzi. Yale wanayonena juu yake kule juu ni wazimu. Naam, hamna kitu kama hicho. Naam, ninyi wanawake pale, lo, ni—ninyi hamwezi. . .Nguo zenu ni nini. . .?" Inafanya hivyo. Biblia ilisema hivyo. "Nywele zenu je, mna zozote. . .?" Biblia ilisema hivyo.

383 Hizo, hizo ndizo tofauti, mnaona? "Msiguse, msishike, msionje." Yeye ni Mungu. Mnaona? Sasa, inamaanisha jambo fulani.

384 Sasa, wao wanafikiri ni kurukwa kwa akili. Bali kwetu tunaoamini na kujua iliyo kweli, tunajua ya kwamba ni Uwepo Wake ulio hai, kwa sababu unafanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani. Amina.

385 "Lo," wao wanasema, "wao huwazia tu ya kwamba wanaona hiyo Nguzo ya Moto." Lo, sivyo! Lo, sivyo! Hatuwazii cho chote.

386 Wao walidhani Paulo aliwazia, pia. Misri ilidhani ya kwamba Israeli waliwazia, bali iliwapeleka kwenye nchi ya ahadi. Naam, bwana! Sisi hatu . . .

387 Waebrania 13:8, mwajua, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele," kama mnayaandika hayo, kuandika, mnaona, ya kwamba, "Ni yeye yule." Si-sio-sio sawa . . . mawazo fulani.

388 Ninapoyaandika haya Maandiko hapa, ninayoandika humu, najua yalipo Maandiko, na hivyo ndivyo ninavyoyaendea. Mnaona?

389 Najua ni Uwepo Wake ulio hai, kwa maana hutenda vile vile katika huyu Roho. Sasa, kama ingalikuwa imeingilia baadhi ya kanuni za imani ama dhehebu, tunajua upesi sana haikuwa Kristo. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Kama ningaliwaelekeza kwenye kanuni fulani za imani ama kitu fulani, kingine, ningalitumwa kutoka kwa dhehebu fulani. Bali mimi siwaletei ninyi kanuni za imani, nami siwafundishi ninyi madhehebu. Ninawafundisha Neno la Mungu, ambalo ni nguvu za kufufuka Kwake Yesu Kristo zilizodhihirishwa, si kwa ajili yangu tu, bali kwa ye yote atakaye. Unaona? Ili ninyi . . .

390 Wewe ni ndugu yangu. Mimi si mtu mkuu, nawe mtu mdogo. Sisi sote ni watu wadogo katika Mungu. Mnaona? Sisi ni watoto Wake wadogo. Hatujui kitu, yale yatupasayo kujua hakika. Yeye hutuacha tujue atakavyo, nasi tunamshukuru kwa yale tunayojua ya baraka Zake. Nami sijishirikishi hili mimi mwenyewe; nataka kulishiriki pamoja nanyi. Mnaona? Nawatakeni ninyi mwe ndani Yake, nami nawatakeni muipokee hii Ishara. Na iwapo hamjafanya hivyo . . . Wengi wenu, karibu ninyi nyote, tayari mmefanya hivyo. Bali iwapo wengine wenu hamjafanya hivyo . . .

391 Unaona, nazungumza katika kanda, pia, mnafahamu. Na nyingi zake . . . Nami sisemi hapa kanisani; sote tumekuja kutoka nje, nakisia. Bali huenda kukawa na maelfu baada ya maelfu watakaoisikia kanda hii, waona. Na, hiyo, ni huduma. Kuna mtu atakayeingia Yeriko kwa siri, mwajua, akiwa na kanda, kwa hivyo tunataka ku—tunataka kumpata yule Mzao aliyechaguliwa tangu awali inapoingia mle, waona, kwa maana ile ghadhabu inakuja.

392 Tunajua ya kwamba ni Uwepo wa Mungu aliye hai, inathibitisha ya kwamba Mungu amekwisha kumfufua kulingana na Neno Lake lililoahidiwa. “Kitambo kidogo na ulimwengu haunioni Mimi tena. Yeriko, Misri, hawataniona Mimi tena. Bali ninyi mtaniona Mimi, kwa maana Mimi . . . ” “Mimi,” neno linalotumka mahali pa jina, ndilo linalorejewa kila mara, unaona. “Mimi nitakuwa pamoja nanyi. Mimi ndiye Ishara. Ufufuo Wangu ndio ile Ishara. Kazi nizifanyazo Mimi zitawatambulisha, zitanitambulisha Mimi ndani yenu.”

393 “Kama ilivyokuwa katika siku za—za Lutu, ndivyo itakavyokuwa Mwana wa Adamu atakapokuja, wakati ule Ujumbe wa jioni utakapotangazwa.”

394 “Kwa maana kutakuweko nuru wakati wa jioni. Karibu tu wakati wa jioni, ile nuru ingekuja.” Loo, Mungu atukuzwe! Yanifanya nijisikie kama kwamba ningalipita mbio katika kundi la askari na kuruka ukuta. Unaona? Unaona? “Yapata wakati wa jioni kutakuweko nuru.” Hiyo ni kweli. Nabii alisema hivyo.

395 “Nitakuwa pamoja nanyi. Nitakuwa katika wakati wa Luther; nitakuwa katika wakati wa Wesley; nitakuwa katika wakati wa Pentekoste; lakini wakati wa jioni kabisa, itakuwa Nuru.” Madhehebu yatatoweka, ndiposa ile Ishara itapakwa. Na wote hawa walio waaminifu moyoni, kupitia kote kule, bila—bila ninyi hawata—hawatakamilishwa. Bali katika ninyi . . .

396 Ni kama vile kichwa kinavyopaswa kwenda, kuchukua mguu. Kichwa hakina budi kwenda, kuuchukua mkono. Kichwa hakina budi kwenda, kuuchukua moyo. Kichwa hakina budi kwenda, kuuchukua mdomo. Unaona. Kichwa hakina budi kwenda.

397 Na sasa tumefikia wakati ambapo ile ishara ilipakwa kwenye kizingiti cha mlango, waona, na kwenye miimo. “Ndiposa nitakapoiona ile damu ikiwa ishara, nitapita juu yenu.”

398 Nitaharakisha sasa, upesi niwezavyo sasa. Yapata tu dakika zingine tano, ama kumi, tutamaliza.

399 Inathibitisha ya kwamba Mungu alimfufua katika wafu. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina”—Mh.] Yeye anaishi kati yetu leo. Na huyo “Mimi” ni Kristo. Na huyo “Mimi” yu pamoja nasi hata mwisho wa . . . Hapo inasema *ukamilifu wa dahari*, ambayo maana yake ni “mwisho wa ulimwengu.” “Nitakuweko hata mwisho wa ulimwengu,” kulingana na Neno Lake lililoahidiwa. Yeye aliahidi hilo. “Na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.” Kwetu si upuzi. Ni Ishara. Ni Ishara.

400 Tunaikubali hii dhabihu takatifu ya Damu. Tunaikubali Damu Yake ya sadaka, kisha tunatoa . . . Yeye anatupa Uzima, ile Ishara, muhuri wa ahadi Yake. Waefeso 4:30, ilisema, “Msiihuzunishe ile damu?” La, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu, ambaye kwa Yeye ninyi” [Ndugu Branham anakoma

kidogo, akiliacha kusanyiko kunukuu, "mmetiwa muhuri,"] "mmefanyiwa agano, mmeachwa..." Mnafanyiwa agano. Mmefanyiwa. Ishara, Roho Mtakatifu, ndiye atakayekuwa muhuri. Wakati cho chote kinapofungwa muhuri, afadhali usiufunje. Hauwezi kuuvunja, wewe, sio muhuri wa Mungu. La. Mnaona? Kwa maana ninyi mme... "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu, wakati huu mwili utakapofufuliwa."

401 Ni mbegu, ishara ya kwamba hiyo mbegu imekwisha tiwa Uzima wa Milele, "*Zoe*, 'Uhai Wangu Mimi,' nami nitaifufua tena katika siku za mwisho." Kisha unapotembea, unajua yakini ya kwamba Uhai wa Kristo umo ndani yako, nawe umo ndani Yake. "Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na kutiwa muhuri mle na Roho Mtakatifu," miongoni mwa waamini hawa hivi, "hata siku ambayo Yesu atakapotufufua." Lo, jamani! Paka Ishara. Hivyo ndivyo inavyomaanisha kwetu. Tunatarajia Sadaka hii kutupa Uzima, nayo hufanya hivyo. Kisha inatupa Ishara, nasi tunapaka Ishara ambayo ni muhuri mpaka...Tukiwa—tukiwa washiriki wa Huyu, ni jambo kubwa vipi, kuwa washiriki, kubatizwa kwa huyu Roho mmoja, kuwa Mwili mmoja wa si-...Mwili wa siri.

402 Je, nilitamka hilo neno sawa, *mythical?* (wa kubuniwa) Wa siri, Mwili wa siri, Mwili wa siri wa Yesu Kristo. Mnaona, Roho Mtakatifu alisema, "Unalitamka vibaya." Sanamu kama mimi, bali Yeye alisema, "Unalitamka vibaya," niliuita, *"wa kubuniwa,"* ambalo ni mwili wa siri wa Yesu Kristo, mwaona, ule Mwili wa siri wa Yesu Kristo. Mimi si...Hatuhitaji elimu; tunahitaji Roho Mtakatifu. Ndiye Pekee. Mnaona? Ndiye Pekee. Naam, mnaona, hiyo labda ilimkwaza mtu fulani mahali fulani, mwanachuoni fulani, basi natumaini amelipata vizuri. Ule Mwili wa siri! Itakuwa kwa ajili kitu fulani, kwa maana hangalisema hivyo. Mnaona? Yeye yuko papa hapa sasa. Yuko papa hapa mimbarani. Yuko huko nje. Ni Yeye. Mnaona? Whiu!

403 Na katika Yeye hamna mauti. Katika Yeye hamna huzuni. Katika Yeye hamna uchovu. Katika Yeye hamna dhambi. Katika Yeye hamna magonjwa. Katika Yeye hamna mauti. Tumo ndani Yake! Shetani akijaribu kukupa kitu fulani, kama magonjwa, chukua Ishara yako na kuipaka. Jamani! Chukua Ishara yako na kuipaka, ya kwamba wewe ni mali iliyonunuliwa ya Yesu Kristo. Ishara inaonyesha ya kwamba nauli yako imelipwa.

Asemapo, "Unapokufa, umepotea."

404 Sema, "Umekosea. Nina mali iliyonunuliwa. Mimi ni mali iliyokwisha nunuliwa. Nina Ishara."

"Ishara ni nini?"

405 Yeye anajua ni nini. Usi-, usicheze naye. Anajua ni nini. Naam, huenda ukanena na baadhi ya hawa wahubiri, nao wangebishana nawe. Si shetani; yeye anajua vema zaidi.

Unaona? Ndivyo, hasa. Yeye aliipinga, mara mbili tatu, mwajua, na kufanya kosa, kwa yale majaribio. Shetani anajua unayonena. Mwonyeshe tu hiyo Ishara, ataruka aende. Naam.

406 Kwa sababu, ni nini? Ni mali iliyotiwa muhuri. Hawezi kuvunja huo, na kutoa kitu mle ambacho ni kizuri. Sema, "Ondoa mikono yako! Mimi nimetiwa muhuri." Lo, jamani! Mali iliyotiwa muhuri! Naam, bwana! Umekwisha kununuliwa. Shikilia Ishara juu ya imani yako isiyotikisika katika ahadi Yake. Mwangalie akiondoka. "Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana!" Unaona? Unaona? Chukua hiyo Ishara. Hilo ndilo kusudi lake. Shetani yuko pale kukujaribu.

Alikuwa Misri, kujaribiana.

407 Kwa nini, unajua, siku hiyo wakati Rahabu alipoweka huyo kahaba . . . Huyo kahaba alipoining'inizia hiyo kamba, hiyo kamba, nakisia baadhi ya hao askari walicheka na kumfanyia mzaha, wakisema, "Huyo mwanamke mzee mwenda wazimu kule juu! Amerukwa na akili. Tazama, anacho kule ndani. Ha, ha, ha! Kwani, uliwahi kusikia mambo kama hayo? Kwa nini, Daktari Yona kasema, hapa, 'Hamna kitu kwa hayo.'" Bali kulikuweko, kwa maana yule mjumbe kutoka kwa Mungu aliuleta ujumbe na akawaambia.

408 Je, ungefikiria hao Wamisri wakisema, "Yaonekana kama . . . Aisee, litazame hilo kundi la watakatifu wafingirikao, wakitia damu! Ha, ha! Si watajichafua, watakapoisafisha hiyo! Lo, jamani! Hizo nyumba kubwa na nzuri, zote zimefunikwa kwa damu! Lo, harufu hiyo! Bila shaka nakwambia itakuwa mbaya sana katika muda wa siku chache. Haitamaanisha kitu. Mnajua kwa nini? Baba mtakatifu *Fulani* alisema hivyo." Bali kulikuweko. Ilikuwako. Ilimaanisha jambo fulani.

409 Inamaanisha jambo fulani kwetu sisi tunaoamini. Waona? Kumbukeni tu imani yenu isiyotikisika mlio nayo katika Neno hili! Sasa, wewe si Hawa tena. Unaona? Wewe si mmoja wa hao wanaotilia shaka, na, vema, kupatana na Shetani. Wewe shikilia kila Neno la Mungu. Unaona?

Hawa alisema, "Vema, Bwana alisema hivyo!"

410 Shetani akasema, "Lakini, unajua, Bwana hakika hatamfanyia jambo kama hilo mtu mzuri kama wewe. Jamani, wewe ni mtu wa kupendeza sana. Yeye hatafanya hivyo." Lo, naam, Yeye atafanya hivyo, pia. Alisema angefanya hivyo.

411 "Vema, baba yangu alikuwa muhudumu. Nimekuwa muhudumu." Si—siwezi kufanya neno. Bila Ishara, umepotea. Ghadhabu iko juu yako, waona, hivyo tu, bila Ishara. Unaona? Naam. Yeye alisema angefanya hivyo, naye atafanya hivyo. Hilo, hilo latosha tu. Amesema atafanya hivyo.

"Lo, naamini siku za miujiza . . . "

412 Naam, bali alisema haikuwa hivyo. “Mimi ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” waona, hivyo ndivyo tu Yeye anavyojithibitisha kuwa.

413 Basi, kwetu sisi, tunajua hivyo. Kwao hao, hawaamini. Bali sisi tunaamini. Tunajua ni kweli. Mnaona?

414 Basi, tukiwa katika hiyo, tunafanyika sehemu ya Neno. Kisha tunachukua ile Ishara, yule Roho, juu ya ahadi, “Mimi ndimi Bwana nikuponyaye.”

415 Sasa jiandaeni kwa ajili ya ibada ya uponyaji usiku wa leo. Unaona? Chukueni ile Ishara, ining’inizeni juu ya Neno, juu ya imani yenu isiyotikiswa katika hilo Neno, atatoka. Sasa, hicho ndicho—Hicho ndicho kitu kinachomwondoa, kwa sababu katika Yeye hamna kitu kama hicho.

416 Ningependa kama ningaliweza kutoa ushuhuda mdogo sasa, juu ya mambo ambayo nimeyaona yakitendeka katika majuma machache yaliyopita. Mnaona? Mnaona? Lo, jinsi ningalishuhudia!

417 Mnajua, pia Luka alisema, “Kama yote aliyotenda Yesu yangaliandikwa katika vitabu, ha. . .hakungalikuweko vitabu vya kutosha ulimwenguni kuyaandika.”

418 Yale tu nimekwisha kuyaona katika huduma yangu mwenyewe, kumwona akiyafanya, haungalivirundika hivyo vitabu juu ya hili jukwaa hapa. Kama ningaliyaandika kirefu niliyomwona Yeye akitenda katika huduma yangu binafsi tu, nikimwona akiyatenda. Mnaona? Yeye alifanikiwa sana katika huduma yangu kuliko katika ile Yake. Sasa, kumbukeni, Yeye alikuwa na ufanisi mwingi sasa, si mimi; Yeye alifanikiwa. Utukufu! Haleluya!

419 Yeye alifanikiwa sana Jeffersonville kuliko kule Nazareti. Alifanya hivyo katika jiji hilo ovu na jiji hili ovu. Amina! Utukufu! Kwa maana, “Yeye hakuweza kutenda miujiza kule,” bali aliifanya hapa. Hatimaye alifaulu, hapa. Alifanikiwa kuifanya hapa. Huenda ilimlazimu kuwapata watu mahali pengine, bali ali—alifaulu kuifanya, hata hivyo. Kwa hivyo, Yeye alifanikiwa sana papa hapa kuliko kule—kule Kapernaumu ama—ama Nazareti, katika hayo. Alifanya miujiza mingi zaidi papa hapa katika Maskani haya kuliko alivyofanya katika huduma Yake Yote duniani. Hiyo ni kweli, aliifanya. Sasa ni vipi ulimwengu ule mwingine? Lo, jamani! Sasa hivyo ndivyo alivyofanya.

420 Sasa kumbukeni, “Yeye” alitenda. Sasa, haikusema nilifanya, mnaona, lo, kwa sababu sikuzifanya. Sikufanya hivyo. Nilimpenda tu na kujitolea Kwake, nikasema alivyosema, kisha Roho Mtakatifu akaenda kwa watu wengine nao wakaamini yale Yeye aliyosema, na halafu Yeye akatenda hiyo kazi. Hivyo tu.

421 Kama anaweza kutufanya sote tuamini! Yeye angefanya nini hivi sasa, kama angeweza kutufanya sote tuamini hivi sasa, sawa? Hakungalikuweko na mtu mnyonge mjini kote. Hiyo ni kweli. Kama angalimfanya kila mtu kuamini, yote yangekwisha. Unaona?

422 Shikilia Ishara yako juu ya imani yako isiyotikisika katika Neno Lake lililoahidiwa, naye Shetani ataondoka.

Sasa nitamaliza sasa.

423 Mungu wakati mmoja alitoa ishara nyingine kwa ulimwengu; ilikuwa upinde wa mvua. Mnakumbuka hiyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye daima, daima amekuwa mwaminifu kwa ishara hiyo, kwa maana aliitoa kama ishara. Maelfu haya yote ya miaka, Yeye hajashindwa kuonyesha hiyo ishara. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Kwa nini? Yeye anaiheshimu. Aliitoa. Aliupa ulimwengu ishara ya kwamba Yeye hatauangamiza ulimwengu tena kwa gharika. Na tangu siku hiyo Yeye daima, daima ameionyesha.

424 Mna vitu fulani hewani, ambavyo huufanya huo upinde wa mvua. Inaponyesha, nalo jua linajitokeza, hiyo huuonyesha. Jua linakausha mvua, kwa hivyo Yeye aliweka upinde wa mvua kule kuthibitisha ya kwamba hakutanyesha mvua ya kutosha duniani kuiangamiza tena. Hilo ni agano Lake. Ni Ishara. Yeye alisema, "Nitawapa ninyi hiyo kama ishara."

425 Yeye aliijali ishara Yake. Aliijali ishara Yake katika siku za Nuhu. Bado angali anaionyesha. Aliijali ishara Yake Kule Misri. Aliijali ishara Yake kule Yeriko. Anaijali siku hizi. Yeye daima huijali ishara Yake inapoonyeshwa.

426 Maelfu haya yote ya miaka, amependa kuonyesha hiyo ishara. Hasahau kamwe. Hasahau ishara Yake. Sasa, haidhuru ulimwengu unabadilika vipi, ule upinde wa mvua ungali pale. Mnaona, Yeye huijali ishara.

427 Hufanya vivyo hivyo sasa, Yeye huijali Ishara Yake. Haidhuru kanisa litabadilika vipi, litafanya *hivi* mara ngapi; Mungu angali anaijali Ishara Yake, hiyo pekee. Inatuonyesha ya kwamba Yeye hakosi kuheshimu yale atendayo, na yale asemayo. Tunakubali na kuheshimu Hiyo. Naheshimu.

428 Yeye anatutarajia pia tumwonyeshe Shatani Ishara Yake juu ya imani yetu, pamoja na vikundi vyake vyote visivyoamini na madhehebu, ya kwamba tunaamini kwamba ahadi Yake ni kweli, naye atafanya alichoahidi kufanya. Hilo ndilo Kanisa.

429 Si ajabu hawawezi kufikia kwenye hatua ya kwanza kule nje, kama tuuitavyo; kunradhi kwa hilo tamshi. Si ajabu hawafikii po pote ila kurudia dhehebu na kufanya kundi la watu waliovalia nadhifu; wenye tabia nzuri, wenye akili, walioelimika. Hawafikii po pote pale, kwa sababu hayo ndiyo wanayoonyesha, "Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mpresbeteri." Hivyo tu ndivyo walivyo.

430 Bali waamini huchukua ile Ishara. Na yale Yesu aliyoanza kufanya kule Galilaya, Yeye anaendelea kufanya sasa kwa kuonyesha Ishara, ya Roho Mtakatifu aliyerudi Kanisani. Kwa kuwa, hayakuwa matendo ya mitume, yalikuwa matendo ya Roho Mtakatifu katika wale mitume, na hiyo ndiyo iliyokuwa Ishara.

431 Wao walisema waliwatambua Petro na Yakobo, walipo-. . . Petro na Yohana, walipopitia kwenye mlango uitwao Mzuri, wakajua walikuwa wasio na elimu. Huenda ikawa walisema, "Pika, halina, mbeba, basua, dafuda, pepa. Nitakwambia juu ya *hili.*" Mnaona? Huenda ikawa kulikuweko sarufi chungu nzima ambazo hawangalifahamu. Huenda ikawa hawakujua tofauti; elimu yo—yote. . . ya hesabu ya Maandiko. Bali iliwabidi hao kutambua ya kwamba hawa walikuwa pamoja na Yesu. Wao waliisha kuonyesha hiyo Ishara, kwa sababu Roho yule yule aliyekuwa juu Yake, kabla ya kusulubishwa Kwake, alikuwa juu yao baada ya kule kufufuka. Amina!

432 Basi hiyo inamfanya Yeye Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Hivyo ndivyo tunavyojua ya kwamba Yeye yu hai. Kwa sababu gani? Tunajuaje ya kwamba tuko hai? Kwa maana Yeye yu hai. Na kwa sababu sisi tunajua ya kwamba tu hai, ni kwa sababu sisi tunafanana naye, na tumo ndani Yake. Naye alisema, "Kwa maana Mimi ni hai, nanyi mu hai pia. Mimi Ndiye," katika Ufunuo, "niliyekuwa nimekufa, nami ni hai hata milele na milele." Na kama—kama tukifa kwa nafsi zetu na tuwe hai katika Yeye, sisi tu hai milele na milele. Kisha Uhai Wake ndani yetu ni kama tu uhai wa cho chote kile, unaonyesha kile alichokuwa. Na hiyo inamfanya yeye yule jana, leo, na hata milele.

433 Sasa wawezaje, wanapoikana Hiyo? Je, hauoni, "kazi zilizokufa"? Mtumikieni Mungu aliye hai, kwa Milele. . . namaanisha, agano la milele la Uzima uliokuwa katika Damu ya Yesu Kristo. Sasa tukiendelea, hata mwisho, mimi. . . Vema, nita-. . . tutamaliza tu. Mnaona, kuonyesha ile Ishara ya neema Yake, upendo Wake! Sasa, bila kupaka Ishara hii. . .

434 Sasa, ni Ishara. Ishara ni nini? Ishara ni dalili ya kwamba deni imelipwa. Bei iliyohitijika imelipwa. Bei ya wokovu wetu ilikuwa mauti, unaona, na hamna mtu angaliweza kuilipia ila Kristo. Na si ro—roho ya kidhehebu, si roho ya papa, si roho ya mtu fulani ama mtakatifu fulani, bali Roho ya Yesu Kristo, juu ya Kanisa, ni Ishara ya kwamba deni imekwisha lipwa naye ametimiza kila sharti alilohitaji Mungu, na sisi pamoja na Yeye tu mmoja. "Siku ile, mtatambua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba Yangu, naye Baba yu ndani Yangu; nami ndani yenu, nanyi ndani Yangu."

435 Ipakeni Ishara! Ipakeni Ishara ya kufufuka Kwake. Hiyo, kwa sababu Yeye alifufuka tupate kuhesabiwa haki, tumekwisha

fufuliwa pamoja naye. Na sasa tunaketi katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, chini ya ushirika wa ile Ishara.

436 Israeli walipoketi pale, huku vilio vikiendelea, mle barabarani, hawakuhangaishwa na cho chote. Jambo pekee, walihakikisha tu ile damu, ile ishara, ilikuwa ikionekana.

437 Hilo tu ndilo jambo linalotupasa kuhangaikia hivi sasa. Kuna shida nji—njiani, inafanyika, marafiki. Haitachukua muda mrefu, shida inakuja. Mnajua hivyo. Hakikisheni ya kwamba Ishara inaonekana wazi. Na Ishara ni Roho Mtakatifu. "Kwa maana kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na kufanywa washiriki wa utukufu Wake," katika Nchi yetu, tunapiga hatua kuelekea makwetu kwenye Nchi ya ahadi.

438 Je, mnapenda? [Kusanyiko linasema "Amina."—Mh.] Mnaamini Ishara? ["Amina "] Wangapi wangetaka kusema, "Lo, Ndugu Branham, niombee, nipate kuja chini ya hii Ishara"? ["Amina."—Mh.]

Na tuviinamishe vichwa vyetu.

439 Bwana Yesu, Mwenye Fadhili nyingi sana! Ulimwengu ulipokuwa dhambini, na hamna mtu hata mmoja angelisaidia, Mungu, katika rehema, akionyesha kimbele, kwa mfano, ya kwamba kungalikuja Ishara ambayo ingaliondolea mbali dhambi, si kufunika tu, bali angaliiondolea mbali. Naye Yesu akaja wakati uliofaa, kisha akamwaga Damu, Uhai Wake Mwenyewe, akichukua...akitufanyia upatanisho kwa dhambi zetu, ndiposa ukamrudisha katika umbo la Roho Mtakatifu, ambaye sasa ndiye Ishara itakayowekwa Kanisani hata atakapokuja. Kwa maana mtume Petro alisema, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa watu wote watakaoitwa na Bwana wetu wamjie."

440 Bwana, kwa neema Yako, msaada Wako, namdai kila mtu atakayesikia huu Ujumbe. Nawadai kwa Mungu, nakuomba Wewe, Bwana, wote walio hapa asuhuhi ya leo na hao watakaoisikiza kanda. Na iwapo kuna mzao po pote, aliyechaguliwa tangu awali, Bwana, kulisikia Neno la siku hizi za mwisho, na waje sasa, kwa uzuri na unyenyekevu, wakaweke zawadi zao msalabani, ama wao wenyewe, kama thawabu ya neema ya Mungu iliyowaita. Na wao wajazwe na Roho Mtakatifu na waonyeshe ile Ishara ya Uhai wa Yesu Kristo katika kufufuka Kwake, mradi tu wangali hapa duniani. Tujalie, Bwana.

441 Maneno haya, Bwana, huenda sikuyasema vizuri. Na iwapo sikufanya hivyo, naomba ya kwamba Roho Mtakatifu atayachukua maneno haya na kuyasema yanavyopaswa kusemwa, watu wapate kufahamu na kujua, bila uovu. Hebu wajue ya kwamba upendo husahihisha. Na wapate kujua ya kwamba ni kwa sababu ya saa tunayoishi, na kule kukaribia kwa kuja kwa Bwana, nasi tunaona zile taa kubwa

nyekundu zikimemetesha, kote ulimwenguni, ya kwamba wakati umekaribia.

442 Watu na wampokee Roho Mtakatifu leo! Nakusihi, nami nawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Na iwe Ishara kwetu mradi tu tungali hai, ambayo uliahidi itakuwa hivyo. Ingekuwa rahisi kuomba hayo, kwa sababu uliahidi itakuwa hivyo, nami najua itakuwa hivyo. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina!

Sasa, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kwa dakika moja.

443 Kwa imani, nikiamini, nimewaombeeni, jinsi nijuavyo, nikiomba kwa weupe wa moyo, kwa yote nijuayo kuombea.

444 Tazameni, najua hayo. Mwajuaje? Mimi huishi kwa zaka na matoleo yenu. Msaada wenu, hapa kanisani, ndio unaonifanya nipate mtu wa kuhubiria. Ni upendo wenu, na "amina" zenu na ushirika wenu. Na maneno yenu mema kati ya walimwengu kule mnakoenda, katika mikoa mbalimbali nchini, ni maneno yenu yanayosaidia kuupeleka huu Ujumbe. Ni ninyi. Sisi ni washiriki katika huu, pamoja na Kristo. Sisi ni ndugu na dada, naye ndiye Mfalme wetu. Nami nawapenda. Mimi—Mimi—Mimi—Mimi, niliko Mimi, nataka nanyi muweko. Mimi huendesha motokaa nchini kote kuzungumza nanyi mara kadhaa. Nataka kukutana nanyi hapa Jumapili asuhuhi. Nawapenda. Nimewapenda daima. Wakati mwingine inanibidi kuwazungumzia kwa ukali sana, bali ni kwa masahihisho tu. Mnaona, ni kwa sababu tu mimi nawapenda, mnaona, nami siwataki muikose. Haiwapasi, haiwapasi kufanya hivyo.

445 Sasa, kwa uzuri na unyenyekevu, kwa yote yaliyo moyoni mwako, kule ndani kabisa, ikubali tu. Sema, "Bwana Yesu, sasa hivi, chukua tu yote yaliyo ndani yangu, yasiyo kama Wewe, na hebu niondolee mbali majivuno yangu yote, yote yaliyo ndani yangu, niyatoe nje. Taka zote, kutokuamini kwote kuliko ndani yangu, na—nakuondolea mbali sasa, Bwana. Nakutupilia mbali. Roho Mtakatifu wa mungu, kama hua, na aingie ndani yangu. Na—nataka kuishi milele, Bwana, nami na—nataka unisaidie wakati huu. Nijalie sasa, Bwana,"

446 Mnapoomba, nasi tutavuma wimbo huu, ama kuimba kwa sauti ndogo, pamoja, *Nampenda*. Kisha, kumbukeni, inakuja kwa upendo, kwa maana Yeye ni upendo. Huku ninapoweka mikono yangu juu ya hizi leso, kwa sababu hao watu huenda wakazipata, kabla haijakuwa usiku.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Nampenda, nampenda.
Kwani alinipenda kwanza, (sasa yatoeni maisha yenu Kwake)
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalva-. . .

447 Mpendeni, mpendeni, mpendeni Yeye. Oneni alivyowatendea. [Ndugu Branham aanza kuuvumisha *"Nampenda"*—Mh.] Ni kwa upendo. Upendo huleta utiifu. Upendo huleta kuposana. Upendo huleta ndoa. Na huko ndiko tunakoelekea, kwenye ile Karamu ya Arusi ya Mwana-Kondoo. Namsikia Mwokozi wangu akiniita, ya kwamba Yeye ananipenda mimi, pia. Mimi, pia! Nam-. . .

448 Kwa moyo wako wote, sikia kitu kizuri sana kikiingia ndani yako. Huyo ni Roho Mtakatifu.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

449 Kama. . .Nitainua mikono yangu, pamoja na wasikizi, kuambatana na muziki, kama nimetenda dhambi, kama nimekosea. . .

Nawaombeeni ninyi sasa, nami mwenyewe.

450 Iwapo nimekosea, mkono wangu Kwako, Bwana, unamaanisha ninasikitika. Mkono wangu Kwako, Bwana, unamaanisha ya kwamba si—sikutaka kufanya hivyo. Nami najua ya kwamba ninakufa, Bwana. Sina budi kuondoka huku ulimwenguni, katika mwili. Nataka kukutana nawe. Mkono wangu unamaanisha, uchukue, Bwana. Nijaze Roho. Nipe Ishara ya upendo Wako juu yangu, Roho Mtakatifu, atakayenifanya niishi vizuri, kwa unyenyekevu, anifanye niishi Maisha yaliyokuwa katika Kristo; kusudi moyo wangu upate kuwaka moto kwa ajili ya watu wengine, hata iwe vigumu kwangu kupumzika, mchana na usiku, hata nitakapompata kila mtu niwezaye. Nitakuwa kama wale wajumbe kule Yeriko; nitamwendea kila mtu niwezaye, nione kama naweza kuwafanya waje chini ya lile agano la Damu, chini ya Damu ya Mwana-Kondoo, wapate kuipokea Ishara.

451 Unaona, Damu husafisha. Roho ni Ishara kwamba Damu imekwisha kutiwa. Mnaona? Roho ndiye Ishara kwamba Damu imekwisha kupakwa. Hadi ile Damu itakapopakwa, Ro—Roho hawezi kuja. Bali Damu inapopakwa, basi Roho ni Ishara, akitumwa kwako, ya kwamba imani yako katika ile Damu imekubalika, nauli yako imekwisha kulipwa. Nauli yako yote tayari imelipwa. Imekwisha. Hiyo kesi imemalizika. Wewe ni Mkristo. Wewe ni mwamini. Kristo yumo ndani yako, nawe umo katika Kristo.

. . . alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

452 Huku mioyo yenu imeinamishwa sasa mbele za Mungu; mchungaji wenu, Ndugu Neville, akiwa na maneno ya kufunga na yale atakayosema.

453 Kumbukeni zile ibada usiku wa leo, ibada ya uponyaji. Njooni mapema. Hebuni tuanze saa moja, hebuni niwe mimbarani saa moja na nusu. Hiyo ni sawa, Ndugu Neville? [Ndugu Neville asema, "Sawa."—Mh.] Sasa tutakuwa na meza ya Bwana, mnaona, usiku wa leo. Njooni!

454 Alasiri ya leo, kaeni Na Huo kabisa. Msiache Ujumbe huu uwaondokee. Kumbukeni, msiache Ujumbe huu uwaondokee!

455 Damu itakuwa Ishara ya kwamba Uhai umekwisha kutolewa. Mnaona? "Kisha nitakapoiona Damu nitapita juu yenu." Roho Mtakatifu ni Ishara ya kwamba Damu imekwisha tiwa moyoni mwako, na ni Ishara ya kwamba Damu imekwisha tiwa. Iwapo haijatiwa bado, basi Ishara haitakuja. Mnafahamu? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Damu sharti ipakwe, halafu Ishara itakuja. Ni Ishara ya kwamba Damu ya ukombozi imekwisha kupakwa na nauli yako imekwisha lipwa. Mungu awabariki. Ndugu Neville.

*Ile Ishara* SWA63-0901M
(Token)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Septemba 1, 1963, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1989 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org